# USAWIRI WA NDOA KATIKA RIWAYA YA *UNAITWA NANI?*

**NA**

**KARINGE JOYCE WARUGURU**

**C50/78844/2009**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI,**

**IDARA YA ISIMU NA LUGHA**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A.) KATIKA KISWAHILI**

**NOVEMBA, 2013**

**UNGAMO**

**TASNIFU HII NI KAZI YANGU BINAFSI NA HAIJAWAHI KUTOLEWA KWA MAHITAJI YA YA SHAHADA KATIKA CHUO KIKUU KINGINE CHOCHOTE**

______________________________ ______________________________

**KARINGE JOYCE WARUGURU** **TAREHE**

**(Mtahiniwa)**

**Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii katika Chuo Kikuu cha Nairobi.**

**WASIMAMIZI**

______________________________ ______________________________

**DKT. AMIRI SWALEH** **TAREHE**

______________________________ ______________________________

**DKT. RAYYA TIMAMMY** **TAREHE**

## TABARUKU

Ninaitabaruku kazi hii kwa familia yangu:

Mume wangu mpendwa, John Gitabi Kimotho,

Mwenzangu katika ndoa kwa karibu miongo mitatu;

Mazao ya ndoa yetu, James Kimotho na Christopher Karinge,

Furaha yangu, chachu yangu, zawadi kutoka kwa Mola;

Wazazi wangu, Marehemu Christopher Karinge na Zipporah Wanjira,

Kwa msingi thabiti mlionipa na kunifunza thamani ya ndoa.

## SHUKRANI

Ninampa Mwenyezi Mungu sifa na shukrani kwa neema zake katika safari hii ambayo imekuwa ndefu na yenye changamoto nyingi. Amenijalia fursa ya kuifanya kazi hii na kuyaridhisha matamanio yangu.

Ninawashukuru wasimamizi wangu, Dkt. Amiri Swaleh na Dkt. Rayya Timammy ambao wamenifaa sana kwa ushauri wao, uelekezi, na zaidi ya yote, uvumilivu wao. Wamenitia moyo hasa, kwa kuweko nilipowahitaji na kunihimiza nilipolemewa.

Wahadhiri wa idara ya Isimu na Lugha wamechangia pakubwa kufanikiwa kwangu. Ndipo nawashukuru Prof. Wamitila, Prof. Habwe, Dkt. Kineene, Dkt. Mbatia, Dkt. Zaja, Dkt. Iribe, Dkt. Mbatiah, Dkt. Mweri na Dkt. Muungania. Kwa njia ya kipekee nawashukuru Dkt. Habwe na Dkt. Mbuthia kwa ushauri wao; na Dkt. Iribe kwa changamoto aliyonipa nikiwa katika muhula wa kwanza, mwaka wa kwanza.

Aidha, nawashukuru wasomi wenzangu kwa ushirikiano wao katika masuala ya kiusomi na ya kijamii. Kwa kweli, wamekuwa marafiki wa dhati kwa kunipa moyo. Hawa ni Lincoln Nyaga, Joyce Murage, Mary Apopo na Pamela Tambasi. Wengine ni Mbula, Kinyua, Mwilaria, Watuha, Kitali, Amos, Mwanjala, Ngunjiri, Njuguna, Too, Mburu, Angela, Timothy, Muhanda, Oluga na Marehemu Jeremiah Mwito Mukaria.

Familia yangu imechangia pakubwa ufanisi huu kwa hali na mali. Namshukuru mume wangu, John Gitabi Kimotho, kwa kuwa mhimili mkuu katika maisha yangu na hali kadhalika, masomo yangu. Pia, nawashukuru wanangu, James Kimotho na Christopher Karinge kwa kunivumilia na kuniunga mkono katika masomo yangu. Ufanisi huu pia, ni zao la bidii ya wazazi wangu, Marehemu Christopher Karinge na Zipporah Wanjira. Baba, Mungu akujalie pumziko la milele. Mama, sipati maneno yanayofaa kuonyesha shukrani zangu kwa kujitolea kwenu, na kuniombea siku zote. Naomba Mwenyezi Mungu akujalie afya na maisha marefu. Nawashukuru pia, wakwe zangu, Lucy na James Kimotho, ndugu, wifi na shemeji zangu kwa kunihimili, nia njema na sala zao. Mungu amjalie neema zake. Nawashukuru pia, Padre Tony Amisssah, Padre Jerome Olianga na

Padre Pierot King kwa kuwa wachungaji wangu, washauri, marafiki na hali kadhalika familia ya kiroho.

Nawashukuru Pauline Mueni na Saveriah Wambui Weru wa *Summit House* kwa kuuchapa muswada huu. Aidha, nawashukuru Polly Nyaga, Joyce Mwangi, Martha Maina, Ambrose Mbugua na Peter Njoroge kwa msaada wao katika kuusanifisha na kuuwasilisha muswada huu. Mungu awabariki kwa utuwema wao.

Sifa na utukufu kwa Mwenyezi Mungu.

# MUHTASARI

Katika tasnifu hii, tumechunguza usawiri wa asasi ya ndoa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* ya K. W. Wamitila (2008). Tunatumia nadharia ya sosholojia ya fasihi kuihakiki riwaya hii. Tasnifu yetu ina na sura tano.

Katika sura ya kwanza tumeeleza tatizo letu la uchunguzi, madhumuni ya utafiti wetu pamoja na nadharia tete. Tumeeleza sababu za kuchagua somo hili na misingi ya nadharia ya sosholojia. Hatimaye, tunachunguza yaliyoandikwa kuhusu somo hili, nadharia ya sosholojia ya fasihi na muhtasari wa riwaya ya *Unaitwa Nani?* (2008). Tumeeleza njia ambazo tumetumia katika utafiti wetu na mwishowe, hitimisho.

Katika sura ya pili tumefiti jinsi asasi ya ndoa imesawiriwa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* (2008) kwa kuchanganua ndoa zilizoko katika riwaya husika na kutathmini mchango wa kila mwanandoa mhusika katika kuiimarisha au kuizorotesha ndoa yake.

Katika sura ya tatu tumezichanganua changamoto zinazoikabili asasi ya ndoa kama zilivyosawiriwa katika riwaya ya *Unaitwa Nani*?.

Katika sura ya nne tumechunguza mikakati ambayo jamii ya riwaya ya *Unaitwa Nani?* inatumia kuikomboa asasi ya ndoa isisambaratike.

Sura ya tano imekuwa hitimisho la utafiti wetu. Tumetathmini kufaulu au kutofaulu kwa utafiti wetu kwa kutathmini matokeo ya uchunguzi wetu, ama yanalingana au hayalingani na madhumuni ya utafiti. Tumeangalia iwapo nadharia tete zetu zimethibitishwa kuwa za kweli au la. Tumetoa mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

## YALIYOMO

MADA........................................................................................................................i

UNGAMO ....................................................................................................ii

TABARUKU ................................................................................................ iii

SHUKRANI……………………………………………………………...……......iv

MUHTASARI.................................................................................................vi

YALIYOMO..................................................................................................viii

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 UTANGULIZI ..........................................................................................1

1.1 TATIZO LA UTAFITI ..............................................................................2

1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI....................................................................3

1.3 NADHARIA TETE ....................................................................................3

1.4 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO ..........................................................4

1.5 UPEO NA MIPAKA YA TASNIFU...........................................................5

1.6 MISINGI YA NADHARIA .........................................................................6

1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO ....................................................12

1.8 NJIA ZA UTAFITI.....................................................................................18

SURA YA PILI

NDOA ZA WAHUSIKA MBALIMBALI KATIKA RIWAYA YA *UNAITWA NANI?*

2.0 UTANGULIZI ...........................................................................................19

2.1.0 NDOA YA KASEKESI NA AGUSTO MURIDHANIA.........................19

2.1.1 MCHANGO WA KASEKESI KATIKA NDOA YAKE.........................21

2.1.2 MCHANGO WA AGUSTO MURIDHANIA KATIKA NDOA YAKE................22

2.2.0 NDOA YA WAZAZI WA KASEKESI ................................................................25

2.2.1 MCHANGO WA MAMA YA KASEKESI KATIKA NDOA YAKE...................26

2.2.2 MCHANGO WA BABAKE KASEKESI KATIKA NDOA YAKE......................27

2.3.0 NDOA YA MWANAMUKA NA KITONGA ......................................................29

2.3.1 MCHANGO WA MWANAMUKA KATIKA NDOA YAKE .............................29

2.3.3 MCHANGO WA KITONGA KATIKA NDOA YAKE NA MWANAMUKA .....30

2.4.0 NDOA YA WAZAZI WA MWANAMUKA........................................................31

2.4.1 MCHANGO WA MAMAKE MWANAMUKA KATIKA NDOA YAKE...........31

2.4.2 MCHANGO WA BABAKE MWANAMUKA KATIKA NDOA YAKE..............31

2.5.0 NDOA YA NYAKOR NA MUME WAKE ..........................................................33

2.5.1 MCHANGO WA NYAKOR KATIKA NDOA YAKE.........................................33

2.5.2 MCHANGO WA MUMEWE NYAKOR KATIKA NDOA YAO ........................34

2.6.0 KAMENE NA CEDDY LUSWETI........................................................................36

2.6.1 MCHANGO WA KAMENE KATIKA NDOA YAKE NA LUSWETI.................37

2.6.2 MCHANGO WA LUSWETI KATIKA NDOA YAKE.........................................38

2.7.0 MUMBO NA MKE WAKE.....................................................................................41

2.7.1 MCHANGO WA MUMBO KATIKA NDOA YAKE...........................................42

2.7.2 MCHANGO WA MKEWE MUMBO KATIKA NDOA YAKE...........................42

2.8.0 DAPHINA NA AMI YA MUMBO ........................................................................44

2.8.1 MCHANGO WA DAPHINA KATIKA NDOA YAKE ........................................44

2.9.0 PASTA NA MKE WAKE .........................................................................................46

2.9.1 MCHANGO WA PASTA KATIKA NDOA YAKE .............................................46

2.9.2 MCHANGO WA MKE WA PASTA KATIKA NDOA YAKE ............................46

2.10.0 KAMINDA MWANA’ A PASTA NA SASI ...................................................... 47
2.10.1 MCHANGO WA KAMINDA KATIKA NDOA YAKE ..................................... 47
2.10.2 MCHANGO WA SASI KATIKA NDOA YAKE ............................................... 49
2.11.0 KASSIM NA WAKE ZAKE ........................................................................... 51
2.11.1 KASSIM NA MKE WA KWANZA .................................................................. 52
2.11.2 KASSIM NA BETTY ........................................................................................ 52
2.12.0 SIR PIPO NA LULU. ........................................................................................ 54
2.12.1 MCHANGO WA SIR PIPO KATIKA NDOA YAKE ........................................ 54
2.13.0 PURUPESA NA TRUVESSA .......................................................................... 58
2.13.1 MCHANGO WA PURUPESA KATIKA NDOA YAKE ..................................... 59
2.13.2 MCHANGO WA TRUVESSA KATIKA NDOA YAKE ..................................... 60
2.14.0 KASINA USINA NA WAKE ZAKE ................................................................... 62
2.14.1 MCHANGO WA KASINA KATIKA NDOA ZAKE ......................................... 63
2.14.2 MCHANGO WA WAKE ZA KASINA .............................................................. 65
2.15 HITIMISHO ........................................................................................................ 66

SURA YA TATU

CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI ASASI YA NDOA

3.0 UTANGULIZI ........................................................................................................ 68
3.1 UKATILI NA DHULUMA ....................................................................................... 70
3.2 UKOSEFU WA MAWASILIANO BORA .............................................................. 74
3.3. WATOTO ............................................................................................................... 77
3.4 KUKOSA UAMINIFU KATIKA NDOA ................................................................ 79
3.5 HILA NA UDANGANYIFU ..................................................................................... 82
3.6 MILA NA DESTURI ZILIZOPITWA NA WAKATI .............................................. 83

3.7 UTANDAWAZI........................................................................................84
3.8 MAGONJWA ..........................................................................................86
3.9 MAHUSIANO YA KIJAMII........................................................................88
3.10 UKOSEFU WA HISIA.............................................................................90
3.11 HITIMISHO...........................................................................................92

SURA YA NNE
MIKAKATI YA KUIOKOA ASASI YA NDOA
4.0 UTANGULIZI ..........................................................................................93
4.1 UWAZI NA MAWASILIANO.......................................................................93
4.2 USHAURI NASAHA..................................................................................94
4.3 MATIBABU YANAYOFAA..........................................................................95
4.4 HISIA KATIKA NDOA...............................................................................95
4.5 MSAMAHA...............................................................................................96
4.7 UVUMILIVU, UELEWANO NA USHIRIKIANO ...........................................97
4.7 THAMANI YA NDOA ................................................................................98
4.8 KUACHA MILA NA ZILIZOPITWA NA WAKATI...........................................99
4.9 UAMINIFU...............................................................................................99
4.10 UHUSIANO WA KIJAMII .......................................................................100
4.11 HITIMISHO...........................................................................................101

SURA YA TANO
TATHMINI NA MAPENDEKEZO
5.0 UTANGULIZI .........................................................................................102

5.1 MADHUMUNI YA UTAFITI....................................................................102

5.2 KUHUSU NADHARIA TETE....................................................................104

5.3 MAPENDEKEZO YA UTAFITI...............................................................105

MAREJELEO ..........................................................................................107

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 UTANGULIZI

Kamusi ya sheria ya *Merriam – Webster* (1996) inatoa fasili ya ndoa kama ile hali ya kuwa mtu ameunganishwa na mwingine wa jinsia tofauti kama mke au mume wake, kwa uhusiano ulio wa kisheria, makubaliano na maagano; na ambao unatambuliwa na kuidhinishwa na sheria, na ambao unaweza kuvunjwa na sheria pekee. *Oxford Advanced Learners Dictionary* (2010) nao wanasema kuwa ndoa ni ule uhusiano wa kisheria uliopo baina ya mume na mke. Ibara ya pili ya sheria za maswala ya ndoa (1962), inaeleza ndoa kama ifuatavyo.

> "Ndoa ni muungano wa kujitolea baina ya mwanamume na mwanamke na kuacha wengine wote.'' (TY)

Kulingana na Collins na Anderson (2006), ndoa ni hali au uhusiano wa kuwa mke na mume. Wanasema pia inaweza kufasiliwa kama muungano wa kisheria au maagano yaliyofanywa baina ya mwanamke na mwanamume kuishi pamoja kama mke na mume.

Katiba ya Kenya (2010:33) katika ibara ya 45 inasema kuwa familia ndicho kiungo cha kimsingi cha jamii na muhimu katika kuleta utaratibu wa kijamii. Pia, inasema kuwa kila mtu mzima ana haki ya kumwoa mtu wa jinsia nyingine, lakini lazima pawe na

makubaliano baina yao wawili. Ibara hii ya maswala ya familia inaeleza kuwa bunge litaunda sheria itakayotambua ndoa zilizofanyika kwa kuzingatia mila, au mfumo wa sheria ya kidini, au sheria ya kawaida. Kwa kuwa mambo mengi katika sehemu hii yanahusu ndoa, tumechukulia kuwa ndoa imetambuliwa katika Katiba ya Kenya (2010) kama msingi wa familia na jamii.

Ndoa ni asasi muhimu ya kijamii kwani kupitia kwayo, jamii inaendeleza kizazi. Lakini wananadharia, na hasa wafeministi, wameisawiri kama asasi inayokumbwa na matatizo mengi.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Tatizo la utafiti ni kuhakiki maudhui ya usawiri wa ndoa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* (2008) ya K.W. Wamitila. Maudhui ni jumla ya mambo yanayozungumziwa katika kazi ya kifasihi. Hujumlisha dhamira, falsafa, itikadi na msimamo. Katika kazi hii tunatafiti maudhui ya ndoa na jinsi yalivyosawiriwa katika riwaya hii.

Asasi ya ndoa inakumbwa na changamoto nyingi sana. Baadhi ya wanaharakati na hasa wafeministi wanadai kuwa changamoto hizi zinatokana na kukandamizwa kwa mwanamke na pia kutazamwa kwake kwa mtazamo hasi. Tunatafiti ndoa ilivyosawiriwa na nafasi ya kila mmoja wa wanandoa katika kuchangia maendeleo au kuzorota kwa ndoa yake.

Kuhakiki maudhui ya ndoa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* sio jambo la sadfa bali ni uteuzi wetu. Hii ni kwa sababu riwaya ya *Unaitwa Nani?* inaangazia mivutano baina ya

wanawake na wanaume katika jamii ya riwaya husika na ambayo yanawakilisha jamii ya leo. Ndoa, kama asasi ya jamii, imechukua nafasi kubwa katika riwaya hii kwani imejadiliwa kwa kina.

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Madhumuni ya utafiti huu ni kuhakiki usawiri wa ndoa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*. Tumenuia kutekeleza yafuatayo:

i) Kutathmini mchango wa kila mwanandoa katika kuboresha au kuzorotesha ndoa yake.

ii) Kubainisha changamoto zinazoikabili asasi ya ndoa.

iii) Kuchunguza dhuluma dhidi ya mwanamume na mwanamke katika asasi ya ndoa.

iv) Kuchunguza mikakati ambayo inaweza kutumiwa kuizuia asasi ya ndoa isisambaratike.

## 1.3 NADHARIA TETE

Nadharia tete za utafiti huu ni:

i) Mbali na wanawake kudhulumiwa katika ndoa, wanaume pia hudhulumiwa.

ii) Kila mwanandoa ana uwezo wa kuiboresha au kuisambaratisha ndoa yake.

iii) Matatizo ya ndoa huwa katika matabaka yote ya watu katika jamii.

iv) Ingawa asasi ya ndoa inakumbwa na changamoto nyingi, inaweza kuzuiwa isisambaratike.

## 1.4 SABABU ZA KUCHAGUA SOMO

Jamii za Kiafrika huthamini ndoa kiasi kwamba, mwanamume ambaye hajaoa au mwanamke asiyeolewa huchukuliwa kama kwamba hajakamilika.Ndoa ni asasi muhimu ya kijamii ambayo inahakikisha kizazi bora kinastawisha jamii (Mbiti 1991: 106). Hata hivyo, asasi hii inaendelea kuzorota. Mada hii imeshughulikiwa na wasomi kadhaa lakini kwa kutumia nadharia ya ufeministi, hasa katika kutafiti usawiri wa mwanamke. Kwa hivyo, mwanamume hubaki kuwa ndiye kiini cha uzoroteshaji wa ndoa, kwa kumdhulumu mwanamke. Aghalabu, mwanamume husawiriwa kama hayawani katili ilhali mwanamke husawiriwa kama kiumbe mnyonge na ambaye daima huchangia kuimarika kwa ndoa yake, na anayehitaji kutetewa na jamii yote dhidi ya ukandamizwaji.

Nyaosi (2008) ametafitia asasi ya ndoa katika riwaya mbili: *Kiu* (Mohamed, 1972) na *Msimu wa Vipepeo* (Wamitila, 2006) kwa misingi ya ufeministi. Katola (2006) amefanya utafiti juu ya dhuluma dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili akitumia nadharia ya ufeministi. Katola (2006), Nyaosi (2008) na Kinyua (2011) wanapendekeza utafiti juu ya dhuluma dhidi ya wanaume ufanywe. Kwa maoni yetu utafiti huu utaziba pengo hili kwa kutomwangalia mwanamume kwa mtazamo hasi, pamoja na kuzibainisha changamoto zinazoikabili asasi ya ndoa na kutathmini uhusika wa kila mwanandoa katika kuistawisha au kuizorotesha ndoa yake anapokumbana na changamoto hizi katika asasi ya ndoa.

Riwaya tuliyoiteua yafaa kwa uchunguzi wetu kwani maudhui ya ndoa yameshughulikiwa kwa kina, na imefanyiwa utafiti na Kinyua (2011) pekee akitumia

nadharia ya ufeministi ilhali sisi tunatumia nadharia ya sosholojia ya fasihi ili kufanikisha malengo yetu. Utafiti wetu utakuwa tofauti na wa Kinyua (2011) kwa kuwa amejikita katika usawiri wa mwanamke, jinsi anavyodhulumiwa na mwanamume na mikakati yake ya kujikomboa ilhali sisi tunatafiti usawiri wa asasi ya ndoa, changamoto zinazoikabili asasi hii na mikakati ya kuiokoa asasi ya ndoa isisambaratike. Utafiti wetu ni tofauti na wa Kinyua (ibid) kwa kuwa tumechunguza changamoto zinazomkabili mwanamume na mwanamke katika asasi ya ndoa, jinsi wanavyokabiliana nazo, na mchango wa kila mmoja wao katika kuiboresha au kuisambaratisha ndoa yake, pamoja na mikakati ya kuizuia asasi hii isisambaratike.

## 1.5 UPEO NA MIPAKA YA TASNIFU

Katika tasnifu hii, tumejikita katika uchunguzi wa maudhui ya ndoa, jinsi ilivyosawiriwa, changamoto zinazoikabili asasi hii na mchango wa kila mwanandoa katika kuboresha au kuzorotesha ndoa yake katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* (2008). Vilevile tumedadisi swala la dhuluma dhidi ya wanaume na wanawake na mbinu za kuzuia asasi hii isisambaratike kwani ndiyo kiini cha jamii.

Hatujajikita katika vipengele vinavyomhusu mwandishi kama vile tabaka lake, jinsia yake, matamanio yake wala hatutajikita katika uchapishaji na usambazaji wa vitabu, bali tumejikita katika mitindo ya uwazaji ya wahusika kuhusu asasi ya ndoa na hisia za kipindi ambamo riwaya teule iliandikwa. Vile vile thamani za hadhira inayolengwa zitarejelewa ili kutathmini kipengele tunachokitafiti.

## 1.6 MISINGI YA NADHARIA

Katika uchunguzi huu, tumetumia nadharia ya sosholojia ya fasihi. Wamitila (2003: 204) anaeleza kuwa nadharia hii hutumiwa na wahakiki au wanahistoria ambao nia yao ni kuthibitisha jinsi kazi fulani ilivyoathiriwa na vitengo fulani vya mazingira kama vile tabaka la mwandishi, jinsia yake, matamanio yake, mtindo wa uwazaji, hisia ya wakati huo, muktadha wa kiuchumi, uchapishaji wa vitabu na usambazaji wa vitabu hivyo, tabaka la kijamii ya hadhira na thamani za hadhira lengwa.

Kulingana na *Encyclopaedia Britannica Online* (2011) mwasisi wa nadharia hii ni Mswisi, Germaine de Stael (1766 – 1817) mwanzoni mwa karne ya 19. Umuhimu wake kifasihi uliibuka katika matini zake *A Treatise of Ancient and Modern Literature* (1803) na *The influence of literature upon society* (1835). Kazi hizi zina wingi wa mawazo mapya na mielekeo mipya. Nadharia tete yake ya kimsingi ni kwamba, kazi ya kifasihi lazima ionyeshe uhalisi wa kimaadili na wa kihistoria, na hali ya kitamaduni, kimaadili, kiroho na kisiasa, na mitindo ya uwazaji ya taifa ambamo kazi ya kifasihi imetungwa.

*Enclopaedia Britannica Online* (2011) wanaeleza kuwa mawazo ya de Stael yalichukuliwa na Hippolyte Taine (1828 – 1893), akayaunda upya na kuyakuza. Kwa sababu hii, anachukuliwa kuwa mwasisi wa nadharia ya sosholojia ya fasihi.

Kulingana na Swingewood (1975:7-9), Taine ndiye mwasisi wa nadharia ya sosholojia ya fasihi na kwa maoni yake, fasihi yafaa kuchanganuliwa kwa kutumia methodolojia inayotumiwa katika nyanja za sayansi asilia. Kwa Taine, fasihi iliakisi jamii na kwa

hivyo yaweza kutumika kama waraka wa jamii ya wakati huo. Alisema kuwa usanii wa kifasihi ulibadilika na kuwa usanii wa uhifadhi wa nyaraka. Taine alimithilisha riwaya na kioo kinachoweza kubebwa popote na ni rahisi kuakisi nyanja zote za maisha na maumbile. Anaendelea kusema kuwa riwaya inawakilisha uhalisi na mkusanyiko wa data ambayo yaweza kuchanganuliwa kwa kuzingatia sheria za kisayansi.

Chalmers (1978: 249 – 256) anaeleza kuwa mawazo ya Taine ni kwamba kazi ya sanaa huamuliwa na jumla ya hali ya kawaida ya mawazo na hali zilizoko katika muktadha wa utamaduni. Chalmers anatoa rai kuwa Taine ndiye mtu wa kwanza kujadili uhusiano wa mwanasanaa na jamii yake na pia wenzake akitumia fomula ya uchaganuzi wa jamii - mazingira – wakati. Anasisitiza kuwa kazi yoyote ya kifasihi ni zao la jamii na ili kuelewa kazi ya kisanaa, msanii au kundi la wasanii, inabidi kuyaelewa barabara mazingira ya kijamii ambamo msanii amekulia. Anaongeza kuwa, matini za kifasihi ni nyaraka za kijamii.

Escarpit (1971: 44) anatoa rai kuwa kabla ya mawazo ya Taine, kulikuwa na wanahistoria na wahakiki ambao walipuuza uhusiano uliopo baina ya jamii na fasihi lakini baada ya Taine, kukawa hakuna upizani tena. Anaendelea kusema kuwa, lazima pawe na kigezo cha kijamii kama hakikisho la ukweli wa kifasihi ambao hukumbwa na mageuzo ambayo anayamithilisha na ramani ya dunia iliyokosa umbo.

Goldmann (1975:6) anatoa kauli kuwa, kuna changanuzi nyingi zinazozingatia uhusiano uliopo baina ya nyanja fulani za fasihi bunifu na uwepo wa uhalisi wa kijamii ambao zinauakisi bila kuubadilisha na kwa uwazi.

Wellek na Warren (1978: 23) wanasema kuwa, kwa kawaida fasihi huibuka ikiwa na uhusiano wa karibu na asasi fulani za kijamii. Kwa sababu hii, inaweza kuwa vigumu kutofautisha ushairi na miviga, uhalisiajabu, kazi au michezo katika jamii za kale. Wanatoa rai kuwa fasihi ina uamilifu wa kijamii ambao hauwezi kuwa wa mtu mmoja binafsi. Kwa sababu hii, maswali mengi ambayo huibuka katika uchanganuzi wa kifasihi aghalabu huwa maswala ya kijamii.

Tutaitumia nadharia ya sosholojia ya fasihi kuyahakiki maudhui ya ndoa kama yalivyosawiriwa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* (2008) kama thibitisho la uhalisi uliopo katika jamii ya karne ya 21.

Nadharia ya sosholojia ya fasihi inaweka wazi uhalisi uliopo katika jamii kwa kuyasawiri mambo vile yalivyo bila kuupendelea upande fulani. Mambo huwasilishwa kama yalivyo katika jamii na kwa hivyo, kazi ya kifasihi huakisi jamii husika.

Kiiru (1978: 100) anasema kuwa riwaya ya Afrika Mashariki inatakiwa iwasilishwe kwa watu, isawiri matamanio yao na kuvunjikiwa kwao katika mabadiliko ya kijamii kwani hawa ndio watu wanaoisisimua jamii. Anaendelea kusema kuwa mwandishi wa riwaya wa Afrika Mashariki anawaandikia watu wake na kwa hivyo mazingira yanayojitokeza ni

yale ya kawaida na lugha inayotumiwa ni sahili, na usawiri wa wahusika uko katika muktadha wa jamii zao. Anaeleza umuhimu wa riwaya kama uzoefu unaotusaidia kujielewa sisi wenyewe na pia kuuelewa ulimwengu tunamoishi, kutambua na kuelewa matatizo yetu na hatimaye, kuwa na matumaini ya kushinda matatizo yetu. Nazareth (1978: xxiv) anaafikiana na Kiiru anapoandika kuhusu majukumu ya waandishi katika nchi zinazoendelea. Anasema kuwa wanariwaya wanapaswa kuisaidia jamii kujielewa na kuyaelewa mazingira yao.

Thiong'o (1978) anaeleza kuwa fasihi ina uhusiano na maisha ya kila siku ya jamii kwani haikui (fasihi) wala kuchipuka katika ombwe tupu. Anatoa rai kuwa fasihi hupewa msukumo, umbo, mwelekeo na upeo na nguvu zinazotoka katika jamii.

Gachukia (1980) anapendekeza nadharia ya kisosholojia kutumiwa katika jamii zilizotawaliwa na wakoloni. Hata hivyo, anasema kuwa nadharia hii inaweza kutumika katika mazingira yoyote ya kijamii kwani inaonekana kuwa na sifa bia.
Zhadnov katika Glicksberg (1987:94) anasema,

> "…Wasanii wa fasihi wanaeleza miono ya halisi ya jamii. Fasihi ni tukio la kijamii, ni mwono wa uhalisia kupitia taswira bunifu."
> (TY)

Eagleton (1988: 469 – 476) anaeleza kuwa kuna sababu mbili za kuutetea mtazamo wa sosholojia ya fasihi. Anasema kuwa jambo la kwanza linatokana na jina lenyewe,

sosholojia ya fasihi. Kwa kweli fasihi halisi inatawaliwa na miktadha yake ya kijamii. Ni lazima mhakiki atilie maanani jambo hili na asipofanya hivyo, uhakiki wake utakuwa dhaifu. Sababu ya pili ni kuwa fasihi amilifu inaumbwa na hali za aina zote. Vilevile, husomwa katika miktadha ya aina zote lakini ni muhimu kuangazia viamuzi vyake vya kijamii.

Rogers (1991) anaafikiana na Griswold (1981) anaposema kuwa, riwaya inaeleza muhtasari na ni kielelezo cha mfumo, ambacho ni cha kipekee za jamii yetu. Riwaya huonyesha jinsi mambo yalivyo na yanavyohisika, yanavyofanywa, yale yanayothaminiwa na thamani yake, na yale ambayo si sawa. Anaendelea kusema kuwa, riwaya husawiri hali changamano za ulimwengu kama zile ambazo huchunguzwa wa wanasosholojia wa kiethnografia.

Cosbey (1997: 227 – 233) ametoa mifano ya wasomi ambao wanatoa rai kwamba sosholojia ya fasihi imetambuliwa kutoka kitambo kuwa inaakisi jamii. Hawa ni Escarpit (1966) na Laurenson na Swingewood (1972). Anaendelea kusema kuwa kwa mujibu wa Fitzgerald (1992), Hendershot na Wright (1993) na Sullivan (1982), wanasosholojia wameutumia usomaji wa riwaya kama njia ya kuwapa wanafunzi wao uhalisi ambao watautumia kuvumbua, kuchambua na kuuelewa ulimwengu wa kijamii. Griswold (1981) katika Cosbey (1997: 227 – 233) anasema kuwa riwaya za leo aghalabu huangazia maswala muhimu ya jamii na zikiwa zimeandikwa kwa ufasaha zaweza kumfanya msomaji kuyaona matukio yaliyomo kama kuwa ya kweli. Anaendelea kueleza kuwa fasihi yaweza kumsafirisha (kiakili) msomaji lakini kwa kawaida, wasomaji wa riwaya

hawapelekwi mbali sana na maisha yao. Kwa maoni ya Cosbey (1997: 227 – 233), riwaya aghalabu huvutia kwa sababu huenda sambamba na tajriba za wanadamu.

Njogu na Chimerah (1999: 29 – 31) wameeleza kuhusu nadharia ya kijamii. Wanaunga mkono nadharia inayofungamanisha fasihi na jamii hasa katika nchi zinazoendelea kwa sababu nadharia hii huthibitisha kuwa fasihi ni kielelezo cha ukweli uliopo katika jamii. Inasisitiza kuwa fasihi ni amali ya jamii.

Kulingana na Ntarangwi (2004: 21) fasihi ni taasisi ya kijamii inayotumia lugha kama mtambo wake kwa hivyo, fasihi huwakilisha maisha kwa upana wake kuhusu uhalisi wa kijamii. Anatoa rai kuwa ikiwa fasihi inalenga watu fulani, basi inahusu jamii fulani. Kama rai hii si kweli basi kutunga kazi hiyo huwa ni kazi bure.

Mbuthia (2005) anaendeleza wazo la Thiong'o kwamba fasihi haichipuki katika ombwe tupu. Anamithilisha maisha ya mtu binafsi na uzi mmoja ulio katika jora kubwa ya jamii. Hivi ni kusema kuwa, mtu huishi katika jamii na kuhusiana na watu wengine katika jamii ili kufanikisha taswira nzima ya jamii hiyo. Kwa sababu hii, wahusika katika kazi ya kifasihi wana umaizi muhimu mno wa jamii zao. Mbuthia (2005:3) anasema kuwa mojawapo ya majukumu muhimu ya fasihi ni kuwasaidia wanadamu kuyaeleza vyema maswala wanayokumbana nayo kibinafsi na pia kama jamii. Pia, fasihi ni chombo kinachoisaidia jamii kujielewa na kuyaelewa mazingira yake.

Akihojiwa na Lutz Diegner juu ya riwaya yake *Bina – Adamu!* katika *Swahili forum 12* (2005: 95 – 97), Wamitila anaashiria kupendelea nadharia ya sosholojia ya fasihi kwani anasema kuwa, ni lazima riwaya ya mwandishi yeyote iakisi mazingira yake, siasa ya nchi yake na mambo mengine ambayo yanamhusu.

Jadhav (2012:67) anasema kuwa kazi ya kifasihi huzingatia na kuumbwa na mazingira yake, viamuzi vya kijamii na thamani za kitamaduni za kipindi hicho.

Baadhi ya wahakiki ambao wametumia nadharia ya sosholojia ya fasihi kuhakiki fasihi ya Kiswahili ni Mbatiah (1999), Orina (2000) na Mbuthia (2005). Mbatiah alitafitia chimbuko na maendeleo ya riwaya ya kitasnifu ya Kiswahili nchini Tanzania. Orina naye alitafitia maadili katika fasihi, akizingatia uandishi wa Shaaban Robert. Mbuthia, naye alitumia nadharia ya sosholojia ya fasihi kuchanganua mtindo na maudhui katika hadithi fupi za Kiswahili. Japokuwa wametumia nadharia ya sosholojia ya fasihi, tafiti zao ni tofauti na utafiti wetu kwa vile tutajikita katika kuhakiki usawiri wa ndoa. Kwa kuwa ndoa ni asasi ya kijamii, nadharia ya sosholojia ya fasihi itafaa uchunguzi huu. Maelezo ya nadharia ya sosholojia ya fasihi ambayo tumeyaeleza katika sehemu hii yatatufaa katika utafiti wetu.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO

Ndoa imesawiriwa na wasanii na wahakiki kadhaa na hasa wafeministi. Germaine Greer, katika *The Female Eunuch* (1970) ameisawiri ndoa kama asasi sumbufu kwa mwanamke. Anawahimiza wanawake kususia ndoa kwa kuwa hali ya kuolewa inawafanya

kumilikiwa na waume wao na hivyo wapoteze utambulisho wao na uhuru wao. Anasema kuwa, si lazima watoto walelewe katika ndoa ya wazazi wao, wanaweza kulelewa na mtu mwingine yeyote. Anapendekeza ndoa za jinsia moja. Katika utafiti wetu tumechunguza jinsi ya kukabiliana na matatizo katika ndoa baina ya mwanamke na mwanamume na hali kadhalika, kuiokoa asasi yenyewe.

Adamson, Briskin na Maphail (katika Wafula na Njogu 2007:93) wakieleza juu ya ufeministi wa kiharakati wanasema kuwa, katika mrengo huu, mwanamume ni adui mkubwa wa mwanamke na uwezo wa mwanamke kuzaa ndio silaha inayotumiwa na mwanamume kuutawala mwili wa mwanamke. Wanapendekeza kama Greer (1970) kuwa, ili wanawake waweze kujikomboa na kujitawala, basi wasiolewe na wanaume lakini washirikiane na wanawake wenzao kimapenzi.

Wafula na Njogu (2007:93) wanasema kuwa kuna vipengele vya utamaduni vinavyomnyima mwanamke fursa ya kutekeleza malengo yake. Miongoni mwa vipengele hivi ni kukosa uwezo wa kuchagua kuwa mke au mzazi wa wanajamii na kuwapo mila na desturi zinazomkandamiza mwanamke asiyezaa. Tunafasiri maana ya vipengele hivi viwili kama ni lazima mwanamke aolewe na azae watoto. Hapa ndoa imesawiriwa kama asasi ya lazima kwa mwanamke na jukumu la mwanamke katika ndoa ni kupata watoto na kuwalea.

Maina (2005: 38 – 40) anasema kuwa hali ya mwanamke kulipiwa mahari anapoolewa, humfanya achukuliwe kama mali ya mumewe na hili ni tatizo kubwa. Gibbe (katika

Maina: 2005) anasema kuwa mahari, yanaviza sauti ya mwanamke kwa mumewe kwani ameshaolewa. Anaendelea kusema kuwa, neno hili ‘kaolewa’ limebeba dhana ‘kanunuliwa’, jambo ambalo haliwezi kufutika. Maina anaendelea kusema kuwa, dhana hii hupatikana katika lugha nyingi za kiafrika katika istilahi kama; ‘ameoa –ameolewa’. Jambo hili hupelekea kugandama kwa mwanamke katika ndoa dhalimu kwani akimwacha mumewe, wazazi wake watalazimika kurudisha mahari iliyolipwa na mume. Mbali na hayo, ni kashfa kwa mwanamke huyu na ukoo wake mzima. Maina anatoa kauli hii anapohakiki nafasi ya mwanamke katika tenzi mbili za Shaaban Robert. *Utenzi wa Hati* na *Utenzi wa Adili* akitumia nadharia ya Ufeministi. Tukitumia nadharia ya sosholojia ya fasihi, tumetafiti ikiwa ndivyo asasi ya ndoa ilivyosawiriwa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*

Kulingana na Momanyi (1998:47) hata ikiwa mambo yamemwendea mwanamke mrama katika ndoa yake, mila na desturi hazimkubalii kumtaliki mumewe. Kwa hivyo, ni vigumu kwa mke kumpa mumewe talaka, jambo linalopelekea wanaume kuwamiliki wanawake. Alikuwa akichunguza usawiri wa mwanamke mwislamu kama unavyobainika katika ushairi wa Kiswahili.

Wamitila (2002: 157 – 158) anaeleza kuwa ndoa kama asasi ya kitamaduni, inaendeleza ukandamizwaji wa wanawake. Imejengwa kwenye msingi wa itikadi ya uwezo mkubwa alio nao mwanamume, naye mwanamke akawa anachukuliwa kama chombo tu.

Osoro (2003: 32 – 36) akihakiki riwaya za Said Mohamed anaakisi maneno ya Germaine Greer kwamba, ndoa ni mojawapo ya asasi za kijamii ambazo zahitaji kuondolewa. Anaendelea kusema ni asasi inayotumiwa kuwadhulumu wanawake kwani wanachukuliwa kama mali au bidhaa kwa sababu wanalipiwa mahari. Akitumia mfano wa riwaya ya *Asali Chungu* (1978) anasema kuwa mwanamke katika ndoa anaweza kuwa huru kiuchumi lakini ateseke kisaikolojia kama vile mhusika Amina katika *Asali Chungu*. Anasema kuwa, baadhi ya wanawake huolewa na wazee kwa sababu wana mali na kwa hivyo, watakidhi mahitaji yao lakini wanawake hawa huingia mashakani katika uzinzi ili kutosheleza ashiki zao, jambo linalopelekea kuvunjika kwa ndoa zao. Pia anasema, kuna dhuluma dhidi ya mwanamke katika ndoa, na aghalabu mwanamke huwa mtumwa wa kumhudumia mwanamume. Anahitimisha kwa kusema kuwa, anayedhurika zaidi katika ndoa yenye matatizo, ni mwanamke.

Katola (2006: 75 – 81) akichunguza udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili, anasema kuwa kwa kuzingatia ufeministi wa Kiafrika, baadhi ya taasisi zinatumiwa kumdhulumu mwanamke na zafaa kubadilishwa au kuondolewa. Anaafikiana na Mbiti (1991: 106) kuwa vizazi vipya hupatikana katika ndoa lakini falsafa ya ufeministi wa kiafrika ni kwamba, mwanamke anapoolewa na kutolewa mahari, anakuwa mali ya mwanamume. Kwa sababu hii, hawezi kumiliki mali, kutoa maoni wala kuelezea kutoridhika kwake. Mume ndiye mwenye mamlaka na ndiye hutoa uamuzi wote. Anasema kuwa wanaume wa Kiafrika, wanatarajia wanawake waliotoshelezewa mahitaji yao waridhike.

Nyaosi (2008) ametafitia taswira ya ndoa katika riwaya mbili za Kiswahili. Hizi ni *Kiu* (1972) na *Msimu wa Vipepeo* (2006). Aligundua kuwa, asasi ya ndoa ina matatizo mengi yanayomkumba mwanamke na hadhi yake katika ndoa, ni ya chini. Yaani, mwanamke ni mshirika nambari ya pili katika ndoa. Ndoa imesawira kama nyenzo inayotumiwa kumdhalilisha mwanamke.

Kinyua (2011: 433) ametafiti jinsi riwaya ya *Unaitwa Nani?* (2008) inavyoshughulikia swala la ukombozi wa mwanamke na aligundua kuwa, asasi ya ndoa ina misingi ya kumpa mwanamume mamlaka mengi juu ya mkewe kiasi kwamba, mwanamume ni mwinyi na mke wake mtumwa. Mwanamke amesawiriwa kama kiumbe duni asiye na akili, kitu cha kumilikiwa na mwanamume. Amefungwa na ndoa na kuyakubali matatizo katika ndoa. Hata hivyo wanawake, wanashirikiana kukosoa asasi za kijamii zinazopinga ukombozi wao. Jambo hili lina athari hasi kwani wanaasi ndoa zao na kulemaza asasi ya familia ambayo ni nguzo ya jamii. Utafiti wake utatufaa kwa kuwa tutatumia nadharia ya sosholojia ya fasihi kutafitia asasi ya ndoa kwa mapana katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* na kulinganisha matokeo yake na yetu.

Wahakiki hawa wote wametumia nadharia ya ufeministi katika utafiti wao, na utafiti wao unaelekea kuegemea upande mmoja katika asasi ya ndoa, yaani kumtetea mwanamke pekee ilhali matatizo ya mwanamume hayashughulikiwi, wala juhudi zake hazitambuliwi. Tumetumia nadharia ya sosholojia ya fasihi ili kuhakiki maudhui ya ndoa kwa kina, jinsi ilivyosawiriwa, bila kupendelea jinsia yoyote, katika jamii yenye mazingira yanayobadilika kwa kasi.

Mbatiah (1999: 190 – 193) akitafiti juu ya chimbuko la riwaya ya tasnifu na maendeleo yake nchini Tanzania ameihakiki riwaya ya Aniceti Kitereza *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Ntulanalwe na Bulihwali (juzuu la kwanza)* anaeleza kuwa watoto ni muhimu katika kuendeleza kizazi. Kwa kawaida, mke ambaye hapati watoto hutalikiwa, anachukiwa na wakwe zake na hana thamani yoyote mbele yao. Pia, kulingana na mila na desturi za Kiafrika kuna baadhi ya kazi ambazo ni mwiko kwa mwanamume kufanya, kama vile kupika. Mbatiah anatwambia kuwa, jambo hili linaonyesha kuwa, kwa mujibu wa mila na desturi hizi, mwanamume hawi kamili bila mke. Kwa kutumia kielelezo cha kisa cha Myombokere na Bugonoka tunaona kuwa, wanandoa wakiwa na upendo, mashauriano na ushirikiano wanashinda matatizo na ndoa yao inafaulu. Mbatiah ameitumia nadharia ya sosholojia ya fasihi kuyahakiki maudhui ya ndoa. Kwa kiasi fulani tutalinganisha utafiti wake na wetu.

Mbuthia (2005: 119 – 125), akichanganua mtindo na dhamira za hadithi fupi za Kiswahili anasema kuwa, katika jamii nyingi za Kiafrika wazazi ndio huziidhinisha ndoa. Vilevile zipo ndoa za kulazimishwa ambazo huwa zimepangwa awali, jambo ambalo linaendelea kufifia katika jamii ambayo inabadilika. Katika utafiti wake, asasi ya ndoa imesawiriwa ikiwa na uzinzi mwingi, kutotosheka katika maisha, matumizi ya dawa za kienyeji ili mmoja (mume) asisinywe na ndoa, kutowajibika, hila, dhuluma na kutelekezwa.

Mbuthia (2005: 125) anasema; “Matatizo ya ndoa ni swala muhimu katika jamii; kwa watu wa rangi zote na matabaka yote.” (TY)

Utafiti wa Mbuthia, umetufaa kwa kuwa ametumia nadharia ya sosholojia ya fasihi kuzihakiki hadithi fupi za Kiswahili nasi tutaihakiki riwaya ya *Unaitwa Nani?*. Tumelinganisha matokeo ya Mbuthia na yetu ili kutathmini ufaafu wa nadharia ambayo tumeitumia.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Kwa mapana, utafiti wetu umekuwa wa maktabani.

Tumeisoma riwaya teule pamoja na kazi nyingine za Wamitila ili tu kupate kufahamu maoni yake kuhusu asasi ya ndoa katika jamii kwa undani. Tumeyasoma maandishi yanayohusu mada yetu na nadharia ya sosholojia ya fasihi katika tasnifu, vitabu na majarida. Tumetumia tovuti kutafitia mada yetu na nadharia ambayo tumeitumia ili kupata mwelekeo bora zaidi katika utafiti wetu. Tumehusisha maoni ya wataalamu wa mada husika, wasimamizi wetu na wasomi wengine.

# SURA YA PILI

## NDOA ZA WAHUSIKA MBALIMBALI KATIKA RIWAYA YA *UNAITWA NANI?*

### 2.0 UTANGULIZI

Katika jamii ya kiafrika asasi ya ndoa inathaminiwa sana kiasi cha kuchukuliwa kuwa lazima kila mwanajamii aoe au aolewe. Pia, ndoa inatarajiwa kudumu mpaka wanandoa wahusika waage dunia. Kwa kuwa asasi hii inawahususisha mwanamke na mwanamume, ni vyema kuchanganua uhusika wa kila mmoja wao katika kuiboresha au kuisambaratisha ndoa yake.

Katika sura hii, tumechunguza jinsi asasi hii imesawiriwa, na mchango wa kila mwanandoa katika ndoa zilizomo katika riwaya hii. Kulingana na Taine (Swingewood 1975:7-9), fasihi huakisi jamii na kwa hivyo, ndoa tunazochanganua ni vielelezo vya ndoa zilizo katika jamii ya riwaya husika.

### 2.1.0 NDOA YA KASEKESI NA AGUSTO MURIDHANIA

Kasekesi ni yatima anayeishi na mjomba wake baada ya kifo cha wazazi wake. Hadithi yake inasimuliwa katika nafsi ya kwanza kwa hivyo, yeye ndiye msimulizi. Anaeleza kwamba, swala la ndoa haliko akilini mwake wakati Agusto anapotaka kumposa. Hii ni kwa sababu siku moja alimshuhudia mama yake akilia na ingawa mama yake hakumpa jibu la kuridhisha, Kasekesi anahisi kwamba kinachomliza mama yake ni matatizo katika ndoa yake. Anamithilisha ndoa na mkimbizano wa paka na panya:

> “Moyoni nikahisi ndoa ni kitu kama ule mchezo wa panya na paka; mzuri ukiwa paka lakini mbaya kama wewe ndiye panya.” (uk.43)

Kabla ya wazai wake kufa, wanampa mawaidha chungu muruwa ya ndoa. Lakini mawaidha ya baba yake Kasekesi yalikinzana na ya mama yake. Pengine jambo hili ndilo linamfanya Kasekesi akose hamu ya kuolewa akiwa katika ujana wake.

Hatimaye, Kasekesi anakubali kuolewa na Agusto baada ya kushawishiwa kwa muda mrefu na Agusto na Mjomba wake. Hata hivyo, hawezi kueleza sababu inayomfanya kukubali kuolewa. Anasema:

> “Kilichonifanya nikubali sijui. Utamaduni, ujinga. uchache wa nadhari, sijui.” (Uk. 43)
>
> “Shinikizo ya mjomba na Agusto wake. Hamu ya kutaka kuyaishi maisha ya ndoa na kwa njia hii labda kumwelewa mama kama alivyoniambia siku moja. Labda ile falsafa ya kulalia kitanda ili kuwajua kunguni wake. Kufungua mlango ili uijue nyumba.” (uk.49).

Ndoa ya Kasekesi na Agusto inaanza kwa harusi iliyojaa shangwe na hoihoi. Ni siku ya furaha kuu inayomfanya Kasekesi kujikaripia kwa kukataa ndoa hapo awali. Hiyo ndiyo siku anayomwona Agusto ametabasamu kwa muda mrefu zaidi. Miezi ya kwanza ya ndoa yao ni ya furaha na anamithilisha maisha yao na mkoko unaoalika maua. Hata hivyo, dhamiri yake inamwonya kuwa ndoa yao ingetumbukia nyongo baada ya biashara ya Agusto kuporomoka.

Ili kuepuka fedheha Agusto anajitumbukiza katika ulevi na hatimaye, anapata ugonjwa wa ini unaopelekea kifo chake. Familia ya Agusto inashuku kuwa Kasekesi anahusika na kifo hicho ingawa walijua hapo awali kuwa Agusto alikuwa mgonjwa. Wanamtesa Kasekesi na mwishoye, wanamfukuza.

### 2.1.1 MCHANGO WA KASEKESI KATIKA NDOA YAKE

Kasekesi anajaribu kusitiri ndoa yao kwa kukataa kutangaza matatizo yaliyomo anapohojiwa na shemeji yake Gitonga. Anamjibu Gitonga, “Si ndoa zote zina matatizo ya kawaida? Hakuna lolote sisi!”(uk. 53). Anachangia ustawi wa ndoa yao kwani hataki kumkashifu mumewe.

Baada ya kupoteza mali yao yote, Kasekesi anakopa pesa kutoka kwa mjomba wake na kuanzisha biashara ndogo ili kukimu mahitaji yao. Kwa hivyo, anachangia ustawi wa ndoa yao, kwani waliweza kupata mahitaji ya kimsingi, pamoja na kuleta amani.

Kasekesi pia anajizatiti kuistawisha ndoa yake kwa kumshawishi Agusto aache kunywa pombe na kumshugulikia kimatibabu alipoanza kuugua.

Jambo hasi ambalo Kasekesi anafanya ni kukubali hali ya ndoa yao kama ilivyo hapo mwanzoni. Hamuulizi Agusto kuhusu safari zake, biashara zake wala marafiki zake. Kwa hivyo hana na ukweli wowote kuhusu mume wake. Anasema:

> "Hakuwa na mazoea na kunieleza undani wa safari zenyewe. Nilichojua tu ni majina ya marafiki zake kama Kassim na Kasina, ambao labda walifanya biashara kama yeye ingawa sikuwahi kuwaona hata siku moja. Sikuona haja ya kumshinikiza kuniambia ukweli wenyewe" (uk. 50).
>
> "Mume wangu alikuja nyumbani usiku mapenzi yetu yalikuwa ya usiku tu. Mapenzi ya giza, mume wa giza, ndoa ya giza."(uk. 61)

### 2.1.2 MCHANGO WA AGUSTO MURIDHANIA KATIKA NDOA YAKE

Agusto anatimiza mahitaji yote ya mkewe mwanzoni mwa ndoa yao kabla ya biashara zake kuporomoka. Kwa hivyo, haipasi mkewe kufanya kazi ila za nyumbani. Kwa sababu

ni tajiri, hataki marafiki zake wamkejeli kwa kushindwa kumtunza mkewe. Kwa njia hii, anaistawisha ndoa yake.

Agusto hamhusishi mkewe katika maswala muhimu ya kifedha kama vile biashara zake na umiliki wa nyumba wanamoishi. Kwa sababu hii, wakati mambo yanapoanza kuwaendea mrama, Kasekesi anashikwa na hofu kubwa. Kutomshirikisha mkewe katika mambo haya muhimu kunaifanya ndoa yao izorote kwa sababu Kasekesi hana uhalisi wa mambo. Hali hii inadhihirika wakati Benki ya Rehani inatuma barua kwa kutolipwa kwa mkopo.

Baada ya kupoteza mali yake, Agusto anajitumbukiza katika ulevi ili kuificha aibu yake. Jambo hili linapelekea kuzorota kwa ndoa yake kwani yeye na mkewe hawakuwa na fedha za kutosha kukidhi mahitaji yao.

> "Akaanza kujiingiza kwenye ulevi uliokubuhu labda akizamisha hicho kiwiliwili chake wasikione na kumcheka. Matokeo yake ikawa hata chakula kupatikana ilikuwa shida." (uk. 54).

Hata baada ya kuonywa na daktari kuwa ini lake liko katika hali mbaya, na kwa hivyo aache pombe, anaendelea kunywa na kutumia visababu kadhaa kwa mujibu wa Kasekesi. Mifano ni;

> “Ule ulevi wa huko alikosema lazima mwanamume aende. Huko kunakozungumziwa masuala ya uwekezaji na maendeleo mbali za masengenyo ya saluni.” (Uk. 55).
>
> “…hata kabla hajaenda shule ya chekechea babu yake alipotengeneza pombe yake ya asali alimwonjesha kidogo. Hii pombe ndiyo ganzi yangu ya joto la akili, ndiyo mzizimo wa kuzimua hali ya maisha….” (uk. 55)

Kwa kutozingatia nasaha ya daktari, kaka yake na mkewe, afya ya Agusto inazorota na hatimaye kufa. Kwa maoni yetu Agusto anachangia kutamatisha ndoa yake.

Jamaa za Agusto wanamshuku Kasekesi kwamba ndiye anayesababisha kifo cha Agusto ingawa kuna na idhibati ya daktari. Kwa sababu, hii wanamtesa Kasekesi sana na kumfukuza.

Baada ya Agusto kupoteza mali yake na kujiingiza katika ulevi, hajali tena jinsi watakavyopata mahitaji ya kimsingi. Kwa mujibu wa maneno ya Kasekesi, anazua fujo anapokuta hakuna chakula. Mizozo baina ya mume na mke huzorotesha ndoa.

Mbali na pombe, Agusto anatumbukia katika uchezaji wa kamari ingawa hana pesa za kufanya hivyo. Kwa hivyo, anaziiba pesa ambazo Kasekesi anapata kutoka kwa biashara aliyoanzisha. Vitendo hivi vya Agusto vinasababisha matatizo zaidi. Kasekesi anasema:

> “Starehe niliyodhani nitapata baada ya kuanzisha banda langu ilikuwa ile ya mbwa kukalia mkia. Agusto akawa anazinyemelea hela zangu kwenda kununulia pombe zake,., au kuchezea kamari ambayo sasa ilikuwa uraibu wake.” (uk. 53)

**2.2.0 NDOA YA WAZAZI WA KASEKESI**

Wazazi wa Kasekesi wanaaga dunia Kasekesi akiwa kijana. Kwa maoni ya wahusika wengine, wazazi wa Kasekesi wanaishi maisha mazuri, na kuwa na ndoa nzuri, mpaka wanaonewa wivu,

> “Kifo cha wazazi wangu hakikuwa cha kawaida, walisema wanakijiji kilitokana na njama za watu wengine waliowalilia ngoa.” (uk. 40).

Hata hivyo, maelezo ya Kasekesi kuhusu mashauri wanayompa unaashiria vile ndoa yao ilivyo.

### 2.2.1 MCHANGO WA MAMA YA KASEKESI KATIKA NDOA YAKE

Mama ya Kasekesi anaonekana kuwa mwenye busara kwani anaisitiri ndoa yake kwa kuficha matatizo walio nayo. Anakataa kumwambia Kasekesi kinachosababisha ugomvi kati yake na mume wake;

> "Akasema kuwa kuna mambo ya watu wazima ambayo siwezi kuyajua katika umri wangu mdogo. (Uk. 42)

Mamake Kasekesi anamshauri binti yake asiolewe na mwanamume mnyamavu. Anasema,

> "Kumbuka pia usimwandame mnyamavu. Hujui amenyamazia nini! Tunaishi katika ulimwengu wa sauti sio wa kimya. Lugha ni silaha kubwa ikiwa utajua kuitumia."
> (uk. 45)

Kutoka kwa maneno haya tunaona kuwa mamake Kasekesi anathamini mawasiliano katika ndoa ili kuweza kupata mawazo ya mumewe na hatimaye, kuafikiana. Hapa anatia juhudi katika kustawisha ndoa yake.

> Kwa kuzingatia maneno yake mama ya Kasekesi, hisia ni muhimu katika ndoa. Anasema kuwa, "…hisia kama hujui ndio chanzo cha uhai wenyewe." (uk. 43)

Kwa maoni yetu anamaanisha kuwa ndoa isiyoongozwa na hisia haina raha kwa sababu anasema:

> "Kwao mwanamke ni kitu cha kumilikiwa na hata kulimwa kama shamba…Ndiyo maana Kasekesi binti, yangu, wanasema hata ardhi ni bikira!" (uk. 44)
>
> "Wanaume wa huku kwetu na mipini yao wanamchukulia mwanamke sawa na ardhi…ni kumbe wa kulimwa!" (uk. 46)

Kwa kumithilisha ndoa na mchezo ambao walio nje wanatamani kuingia na kucheza vizuri zaidi ya waliomo ndani, inaonekana kuwa ndoa ya wazazi wa Kasekesi ina na matatizo kiasi cha mamake Kaekesi kujuta,"Ingelikuwa leo, ningeliishi peke yangu." (uk. 46).

### 2.2.2 MCHANGO WA BABAKE KASEKESI KATIKA NDOA YAKE

Kutokana na ushauri wa wazazi wake, Kasesekesi anapata kumfahamu baba yake na kuthamini mchango wake katika ndoa yake. Babake Kasekesi anaonekana kutawaliwa na mila na desturi zilizopitwa na wakati. Anakataa kubadilika jinsi utamaduni unavyobadilika kutokana na ushauri wake kuwa mwanamume ndiye kichwa cha nyumba, ndiye anayemtunza mwanamke katika maisha yake; ndiye anayemwelekeza akienda kombo; na kumwelekeza bibi yake jinsi ya kuishi na wengine. Anaongeza kuwa lazima

mwanamke amnyenyekee mumewe ili maisha yake yawe bora. Kwa kuwa babake Kasekesi anatawaliwa na itikadi hizi alichangia kuzorotesha ndoa yake.

Kwa kushikilia utamaduni uliopitwa na wakati, babake Kasekesi hamthamini mke wake wala kumheshimu katika anasema;.

> "Ni kweli binti yangu, wala usiyasikilize maneno lipyoto wanaodai kuwa jamii yetu inamdharau mwanamke. Hasa mamako, unasikiaaaa!" (uk 48)

Hapa anamwita bibi yake lipyoto. Longhorn (2011:267) wanatoa fasili ya lipyoto kama mtu anayezua vurugu baina ya watu. Kwa hivyo, babake Kasekesi ana mtazamo hasi wa mke wake.

Inaonekana kuwa anaunga mkono kuadhibiwa kwa wanawake katika ndoa anaposema;

> "Wanaume wa huku kwetu wanamtunza mwanamke vizuri mradi usiwe na kichwa kigumu. Ukiadhibiwa kwa kuwa na utundu wa mkia wa nguruwe usirudi hapa!" (uk 48)

Yawezekana kuwa hapo awali Kasekesi anapwona mama yake akitoka chumbani akilia, na kusikia baba yake "akiguta humo ndani kama fahali aliyefungiwa zizini" (uk 42), babake amempiga mama yake. Tendo hili linazoretesha ndoa ya wazazi wa Kasekesi.

### 2.3.0 NDOA YA MWANAMUKA NA KITONGA

Kitonga ni mfanyi biashara wa kimataifa anayemuoa Mwanamuka, msichana kutoka jamii maskini. Kitonga alikuwa ameachana na mke wa kwanza ilhali Mwanamuka ni msichana wa umri mdogo ambaye hajafanikiwa kupata elimu ya shule ya sekondari kwa ajili ya umaskini kwa hivyo, wana tofauti kubwa ya umri. Mahari anayolipiwa Mwanamuka ni mbuzi watatu. Mama yake anapewa pia, kiasi fulani cha fedha ambazo anazitumia kugharamia elimu ya ndugu zake Mwanamuka.

Ndoa ya Kitonga na Mwanamuka inavunjika baada ya miaka michache kwa ajili ya Mwanamuka kukosa kutunga mimba.

### 2.3.1 MCHANGO WA MWANAMUKA KATIKA NDOA YAKE

Miaka mitatu baada ya kuolewa, Mwanamuka hakufanikiwa kutunga mimba, na swala hili linazua fujo katika ndoa yao. Anafanyiwa uchunguzi na daktari wao lakini hapatikana na ila. Kuchunguzwa kimatibabu ni juhudi yake ya kuiimarisha ndoa yake.

Jamaa za Kitonga wanamdharau Mwanamuka kwa sababu hazai, na wanamkejeli na kumtusi. Mwanamuka hagombani nao, hasa Kenzi, dada yake Kitonga, bali anajaribu kujadiliana naye kwa unyenyekevu na uvumilivu. Hata Kenzi anapomfahamisha kuwa msichana wa kazi ana mimba ya Kitonga, Mwanamuka hatumii lugha ya matusi. Anajaribu kuiimarisha ndoa yake kwa kuwa mume wake, Kitonga, hangemwuunga mkono bali angewaunga mkono jamaa zake.

Kwa maneno ya msimulizi, hata baada ya kitumbua cha Mwanamuka kuingia mchanga, anajaribu "…kusimama tisti kuitetea, kuipigania ndoa yake" (uk. 70) Ingawa haijaelezwa anaitetea na kupigania ndoa yake vipi, ni wazi kwamba anatia juhudi kuistawisha. Hata hivyo, juhudi zake hazifanikiwi.

### 2.3.3 MCHANGO WA KITONGA KATIKA NDOA YAKE NA MWANAMUKA

Kitonga anamuoa Mwanamuka baada ya kuachana na mkewe wa kwanza. Msimulizi anasema kuwa pengine ilikuwa njia yake ya yakisaikolojia ya kujihisi kijana. Baada ya miaka michache bila ya kujaaliwa kupata mtoto, anamlaumu mkewe, kuwa ndiye mwenye ila. Baada ya Mwanamuka kutopatikana na kasoro naye kushauriwa kufanyiwa uchunguzi, anakataa na kuendelea kumlaumu Mwanamuka. Ingawa Kitonga anadai kuwa ameshapata watoto kabla ya kumuoa Mwanamuka, kuna uwezekano kuwa yeye ndiye ana kasoro kwa kuwa msimulizi hajataja ikiwa kuna watoto wa Kitonga na mkewe wa kwanza. Pia, hakuna thibitiso kuwa mimba ya mjakazi ni yake Kitonga kama inavyodaiwa. Kwa kukataa kufanyiwa uchunguzi na kumlaumu mkewe kwa kukosa kutunga mimba, Kitonga anaisambaratisha ndoa yake kwani hachangii kutafuta tatizo liko wapi na hatimaye, jinsi ya kulirekebisha.

Kitonga anawaachalia jamaa zake kumdharau Mwanamuka, kumtusi na kumpiga vijembe. Hata msichana wa kazi anapopata mimba, Kitonga anamtuma Kenzi, dada yake, akamjulishe Mwanamuka. Kitendo hiki kinaizorotesha ndoa yake kwani anawapa jamaa zake mamlaka juu ya mke wake, wakamtendea walivyotaka, wakamdunisha.

Kutokana na ujumbe unaoletwa kwa Mwanamuka na Kenzi, inadhihirika kuwa Kitonga ana uzoefu wa kumdanganya Mwanamuka anaenda nyumbani ili akamsaidie msichana wa kazi, ilhali ziara yake ni ya kimapenzi. Zaidi ya uongo, Kitonga anashiriki katika uzinzi na msichana wa kazi ambaye anashika mimba. Anatia ndoa yake najisi. Hata hivyo, kuna uwezekano kuwa mimba anayoishika kijakazi si ya KItonga. Vitendo hivi vya Kitonga vinatikisa ndoa yake na Mwanamuka na hatimaye kuivunja. Kwa hivyo, Kitonga anaisambaratisha ndoa hii.

**2.4.0 NDOA YA WAZAZI WA MWANAMUKA**

Wazazi wa Mwanamuka ni mafukara. Walitumaini kuumaliza ufukara kwa kuwaelimisha watoto wao. Ndoto hii haikutimizwa kupitia kwa Mwanamuka kwa sababu jamaa ambao wangewasaidia wanachukulia kumwelimisha msichana kama uwekezaji mbaya.

**2.4.1 MCHANGO WA MAMAKE MWANAMUKA KATIKA NDOA YAKE**

Mama yake Mwanamuka ndiye anayeonekana kutia juhudi za kukata duru ya ufukara na kuiinua hadhi yao kwa sababu ndiye anahangaika huku na kule akitafuta mfadhili wa kumlipia Mwanamuka karo. Pia, msimulizi anatuambia kuwa wakati wa kuandaa ndoa ya Mwanamuka, mama alipewa fedha za kugharamia elimu ya wadogo zake. Kushughulikia maendeleo ya watoto ni mchango chanya katika ndoa yake.

**2.4.2 MCHANGO WA BABAKE MWANAMUKA KATIKA NDOA YAKE**

Mwanzoni, baba yake Mwanamuka anaonekana kushirikiana na mama yake Mwanamuka kuikimu familia yao:

> "Wazazi wake, ambao walikuwa wakipanda miche katika msitu wa Mapadre…walishindwa na karo ya shule. Ndoto yao waliyokuwa nayo ya kuvunja duru ya umaskini ikawa inayeyuka kama barafu iliyotiwa kwenye tanuri." (Uk. 62-63)
> "Waliwaendea jamaa zao kuutaka msaada." (uk. 63).

Kushirikiana kwa babake Mwanamuka na mkewe kulichangia kustawishwa ndoa yao.

Baadaye, babake Mwanamuka alimwachia mke wake shughuli ya kuupata msaada wa kugharamia elimu ya Mwanamuka.

> "Mamake Mwanamuka, ambaye ndiye aliyekazana kuupata huo msaada, maanake babake, keshazama kiwiliwili na kinywa kwenye mapombe ya kijijini, kidogo alichopata kinamezwa na pombe au na vibiritingoma wanaomwimbia sifa za uongo." (uk. 63)

Kutumia fedha zake chache katika ulevi kulichangia kuzorotesha ndoa yake. Pia, kuna uwezekano kuwa kwa ushirikiano wake na "vibiritingoma", alitia ndoa yake najisi kwa uzinzi, na hali kadhalika kusambaratisha ndoa yake.

**2.5.0 NDOA YA NYAKOR NA MUME WAKE**

Nyakor alikuwa msichana kutoka familia fukara na alilelewa na mama yake, ambaye alifanya kazi ya uvuvi. Nyakor alikuwa mwerevu sana shuleni lakini mama yake alikufa akiwa hajamaliza masomo ya shule ya upili. Kwa sababu hii alipata ari mpya na kufuzu hadi chuo kikuu alipopata shahada ya somo la uhandisi wa umeme. Nyakor aliolewa na mhandisi wa mitambo ambaye hakupenda utani. Ndoa yake ilianza kuzorota miaka kadhaa baada ya Nyakor kuwa na uvimbe kwenye ziwa lake kwa miaka miwili. Baada ya kuvutana kwa muda, ndoa yao iliisha kwa ghafla baada ya mume wa Nyakor kufa kwa ajali ya barabarani.

**2.5.1 MCHANGO WA NYAKOR KATIKA NDOA YAKE**

Baada ya kufunga ndoa yao, Nyakor alipata kujua kuwa mume wake hakupenda utani wala mizaha. Ingawa Nyakor aliipenda sana, aliamua kuiacha ili aweze kupatana na mume wake. Huu ni mchango chanya wa kuistawisha ndoa yao.

Ziwa la Nyakor linapokatwa ijapokuwa inabainika kuwa halina saratani baada ya kufanyiwa uchunguzi, mume wake Nyakor anaanza kukosa nyumbani. Kwa hivyo, Nyakor hapati faraja kutoka kwa mume wake kama hapo awali. Anahisi kuwa ndoa yao imechukua mwelekeo wa kuporomoka, na kumpendekezea mume wake wamuone

mtaalamu wa kisaikolojia kwa ushauri nasaha kuiokoa ndoa yao. Hii ni juhudi chanya kuiimarisha ndoa yao.

Mume wake Nyakor anapokuwa amelewa sana baada ya siku kadhaa za kutowasiliana na uhusiano mbaya, anataka wayaendeleze mapenzi yao. Nyakor naye anamueleza jinsi ya kustawisha mapenzi katika ndoa, lazima kuzikuza hisia za mapenzi na kuzistawisha. Alitia juhudia kuistawisha ndoa yao.

### 2.5.2 MCHANGO WA MUMEWE NYAKOR KATIKA NDOA YAO

Mume wake Nyakor ni mwenye tabia nzura ila yeye hapendi utani. Ingawa mkewe anaupenda utani, yeye haulegeza msimamo wake ili waweze kupatana. Kumfanya mwenzake aache anachopenda ni jambo hasi katika ndoa yao.

Baada ya Nyakor kupata uvimbe katika ziwa lake, mume wake anatenga fedha za kugharamia matibabu yake. Hii ni juhudi chanya katika kustawisha ndoa yao.

Hata hivyo bwana huyu anazitumia fedha anazozitengea matibabu ya Nyakor kwa kulipia deni. Kwa kuwa na wasiwasi, Nyakor anaenda kutafuta matibabu katika hospitali ya umma ambako daktari anapendekeza ziwa litolewe bila kufanya uchunguzi wa kina. Uchunguzi wa baadaye unathibitisha kuwa ziwa halina saratani. Mumewe Nyakor hakuwajibika kuzihifadhi fedha za kugharamia matibabu ya mkewe na hivyo ndiye aliyesababisha Nyakor kupoteza kiungo muhimu sana cha mwili muhimu sana. Jambo, hili linampa Nyakor uchungu mwingi.

Mume wa Nyakor anaanza kuwa adimu nyumbani badala ya kumfariji Nyakor kwa kupoteza titi lake. Hii ni kinyume na alivyokuwa akifanya awali. Kutomfariji mke wake kunaisambaratisha ndoa yao.

Nyakor ananpendekezea mumewe watafute ushauri kwa mtaalamu wa kisaikolojia ili kuinusuru ndoa yao inayoelekea kuangamia lakini mumewe anakataa. Kwa kukataa kwake, ndoa yao inaendelea kusambaratika.

> "Nyakor akasisitiza kuwa ni bora wakamuone mtaalamu wa kisaikolojia; angeweza kuwasaidia kuinusuru mashua yao ya ndoa ambayo ilikuwa inasogea kwenye kiini cha mto wa maisha.Lakini mumewe akagomea kama mpiga kafi anayejitahidi kupiga kafi kwa wepesi kupambana na mawimbi yanayosukumiza mtumbwi wake kwenye mteremko. Akasema hawezi kumwendea mwanamume mwenzake kumtaka ushauri wa jinsi ya kuishi" (uk. 78-79).

Mumewe Nyakor anataka wayaendeleze mapenzi yao baada ya kipindi cha kutowasiliana, Nyakor akamwambia ni muhimu kwanza kuziibua husia za mapenzi lakini mumewe anasema kuwa uhusivu wa ujana hauna nafasi katika ndoa. Anamithilisha mapenzi katika ndoa na moto wa kifuu, ambao hauonekani. Mtazamo huu wa mumewe Nyakor ni hasi kwa ndoa yao kwa sababu mahusiano baina ya mume na mke huuhitaji uhisivu ili kuridhisha.

Mitazamo tofauti ya mapenzi baina ya Nyakor na mumewe inazusha ugomvi kwa sababu Nyakor anasema kwa kiingereza na kutumia istilahi ya utaalamu wa mumewe. Anasema,*"It is so mechanical…!"*(uk. 79)

Mume wake Nyakor andhani mukewe anaidharau taaluma hiyo. Anashikilia hilo na kukataa kubadilisha msimamo. Tukio hili linapelekea kusambaratika kwa ndoa yao:

> "Utando mwepesi wa kovu lao ukaumbuka
> na kuonyesha wekundu wa nyama unaotia
> unyenyezi.(uk.80)

**2.6.0 KAMENE NA CEDDY LUSWETI**

Kamene ni msichana anayechukiwa na baba yake baada ya kuzaliwa kwa vile baba yake anatarajia mvulana. Akiwa bado na umri mdogo, baba yake anamuoza kwa mzee mmoja, mnywaji pombe na kuyakatiza masomo yake. Anatorokea kwa mwalimu wake ambaye alimsaidia kuendelea na elimu. Anasoma hadi akapata shahada ya uzamili na kuwa mwalimu wa chuo cha walimu. Kutokana na ndoa yake mzee, anachukia ndoa na

kuchelea kuwa na uhusiano ambao ungeishia kwa ndoa. Hata hivyo mawazo yake yalibadilika kwa kutangamana na Ceddy Lusweti. Uhusiano wao unaishia kwa ndoa ambayo inavunjika baada ya miaka michache.

### 2.6.1 MCHANGO WA KAMENE KATIKA NDOA YAKE NA LUSWETI

Kamene alifikiri kwa kuwa Lusweti alikuwa na tajribu ya ughaibuni, alikuwa ameuacha utamaduni wa jamii yake na kuwa na mtazamo mpya wa maisha na kwa hivyo akakubali kuolewa naye.

Baada ya kuolewa, Kamene anamweleza Lusweti kwamba mama yake hastahili kuwa na mamlaka makubwa kama kabla ya ndoa yao. Hii ilikuwa juhudi ya kuiimarisha ndoa yao kwa sababu yeye anastahili kutimiza wadhifa wake kama mke kama vile kumfulia Lusweti nguo zake, na kushauriana naye juu ya masuala ya familia yao.

Kamene anatia juhudi katika kustawisha mawasiliano baina yake na mume wake ili kusuluhisha matatizo. Mfano ni Lusweti anapoanza kutowewa nyumbani baada ya Kamene kushika mimba.

Wakati Lusweti anataka kutoka nyumbani baada ya kumtoa Kamene na mtoto hospitalini, Kamene anajaribu kumshawishi kwa maneno asitoke bali akae nyumbani. Kamene anadhihirisha hisia zake, jambo ambalo ni muhimu katika kustawisha ndoa.

Juhudi nyingine Kamene anayotia katika mawasiliano ni wakati Lusweti anapomzaba kofi kwa kuchelewa kumpakulia chakula. Kamene anajaribu kuongea naye kwa upole na hata kumwita *"Darling"*. Ndipo baada ya mawasiliano haya, Lusweti anajifanya ameona makosa yake na kuomba msamaha.

Usemi ufuatao wa Lusweti unaashiria kuwa Kamene alikuwa amependekeza jinsi ya kuboresha mahusiano yao ya kimwili kama kabla ya kufunga ndoa.

> "Mambo hayo yalikuwa ya zama zile kwenye ndoa mambo yanaenda kwa ada..ni kama ibada za jeshi..kila kitu mahali pake!..." (uk. 97)

### 2.6.2 MCHANGO WA LUSWETI KATIKA NDOA YAKE

Baada ya kumwoa Kamene, Lusweti hampi nafasi yake kama mke wake ila anaendelea kumpa mama yake mamlaka makubwa kuyahusu maisha yake. Kamene anajaribu kumfahamisha Lusweti kuwa si vyema lakini Lusweti anashikilia msimamo wake, ambao una athari hasi katika ndoa yao kama inavyodhihirishwa na madondoo yafuatayo.

> "Chochote alichotamani kufanyiwa, hata kiwe ghali kiasi gani, au kiwe kinahusisha mshahara wake wote, Lusweti hakuweza kumvunja moyo mamake, hata kama itakuwa na maana kuwa itabidi waahirishe mipango yao wenyewe." (uk 96)

> "...kwa kusema kuwa katika maisha yake hajasikia "mwanamume kuulizwa alikuwa wapi". Hata mamake ('ah mamake tena') hakuwahi kumwuliza babake anatoka wapi." (uk. 97)

> "Kamene alikuwa ameagizia mumewe amfahamishe rafiki yake mmoja shule amtafutie msichana wa kazi. Lakini hakufanya hivyo, alisema mamake aliahidi kushughulikia hilo. Lakini alipofika nyumbani, mamamkwe hakuwa ameshughulikia hilo asilani." (uk 98.)

Uhusiano baina ya Lusweti na Kamene unaanza kudhoofika muda mfupi baada ya kufunga ndoa; hata mahusiano yao ya kimwili yanakosa hisia. Kamene anapojaribu kuzua hisia, Lusweti anamwambia;

> "Mambo hayo yalikuwa ya zama zile….kwenye ndoa mambo yanaenda kwa ada…" (uk. 97)

Hakutaka kutia juhudi yoyote.

Lusweti alianza kuadimika nyumbani Kamene anaposhika mimba. Anamwacha Kamene peke yake na "…kwenda kuwachekesha wengine." Kwa maoni yetu, "wengine" ni wanawake Lusweti anaohusiana nao nje ya ndoa. Anaisambaratisha ndoa yake.

Kwa ajili ya kutoweka nyumbani, Kamene anamuuliza Lusweti ambaye anakasirika sana na kutoweka zaidi. Anachangia pakubwa kuisambaratisha ndoa yake kwa kutoshiriki katika mawasiliano baina yake na mkewe ili kusuluhisha matatizo.

Anapomtoa Kamene na mwanawe hospitali, anawaacha nyumbani bila yeyote wa kuwasaidia (na hata anaporejea nyumbani anataka kuhudumiwa na mke wake. Hajali kuwa Kamene amejifungua kwa njia ya kufanyiwa upasuaji. Lusweti kama mume hajali wala kuwajibika.

Lusweti ni katili kwa sababu mbali na kutomsaidia wala kumwuguza mkewe, anamchapa; mara ya kwanza kwa sababu ya kuchelewa kumwandalia chakula, na mara ya pili kwa sababu ya kumnyoa mtoto, kinyume na desturi ya jamii ya Lusweti. Ukatili wake unadhihrika Kamene anapompigia simu kumwambia kuwa mtoto ni mgonjwa. Anasema,

> "…atapona kama ana uwezo wa kuhimili ugonjwa wenyewe. Asipopona ndiyo hivyo." (uk. 107)

Ukatili wa Lusweti unasambaratisha ndoa yao. Ni baada ya kumpiga Kamene mara ya pili ambapo uhusiano baina yake na mke wake unadhoofika zaidi. Msimulizi anasema,

> "Na tangu siku hiyo ndoa yao ikaingia ganzi
> kubwa iliyowanya wote wawili kuvikunja
> viganja vyao." (uk.103)

Lusweti anajitokeza kama mtu ambaye anayosema ni kinyume na yale yaliyo moyoni mwake. Ana sifa ya uigizaji ambayo ina athari hasi katika ndoa yake. Anajitia kumwomba Kamene msamaha baada ya kutomsaidia na kumpiga lakini habadilishi mwenendo wake. Anatishia kumtorosha mtoto wao, Lilith, ingawa hapo awali anamchukia na kutomjali.

**2.7.0 MUMBO NA MKE WAKE**

Mumbo alikuwa ameapa kuwa hataoa maishani mwake. Aliathiriwa na matukio mawili ya uzinzi aliyoshuhudia. Baba yake anampa mawaidha kuhusu ndoa na wanawake lakini Mumbo hana nia ya kuoa. Anampuuza baba yake kwa kuwa anafikiri baba yake hajajitayarisha vyema kuishi maisha ya ndoa. Hata hivyo, Mumbo anaingia katika ndoa bila kujitayarisha vyema. Anasema kuwa anjipata katika ndoa kama ajali. Ndoa yao inavunjika baada ya yeye kuipoteza kazi yake, jambo linalopelekea mke wake kutomthamini.

### 2.7.1 MCHANGO WA MUMBO KATIKA NDOA YAKE

Baada ya kujikuta katika ndoa, Mumbo anakubali hali hiyo na kutia juhudi kuiboresha ndoa yake kwa njia tofauti.

Anapofanya kazi katika kiwanda cha mafuta, anatosheleza mahitaji ya familia yake. Katika kipindi hiki cha ndoa yao kuna amani, baina yake na mkewe.

Mumbo pia, anaweka akiba ya fedha anapofanya kazi katika kiwanda cha mafuta. Fedha hizi zinaisaidia familia yake baada ya yeye kuachishwa kazi. Hii ni busara inayoiboresha ndoa yake.

Anatia juhudi kuzunguka huku na kule kutafuta kazi baada ya kupoteza kazi yake. Pia anaupeleka mswada wake kwa wachapishaji, kuufanyia marekebisho na hata baada ya kuharibiwa na maji ya mvua, hakati tamaa. Hii ni juhudi ya kukidhi mahitaji ya familia yake na hali kadhalika kuiimarisha ndoa yake.

Mumbo anajitahidi kuimarisha mawasiliano baina yake na mke wake kwa uwazi.

### 2.7.2 MCHANGO WA MKEWE MUMBO KATIKA NDOA YAKE

Mke wa Mumbo amesawiriwa kama anayemtegemea Mumbo pakubwa ili kukidhi mahitaji ya kimsingi. Kwa sababu hii, Mumbo anapopoteza kazi yake, maisha yanasambaratika. Hili linatokea kwa sababu mke wake alitarajia kufanyiwa kila kitu (uk. 159).

Mke wa Mumbo ana mawazo hasi kumhusu Mumbo. Haamini kuwa Mumbo anajitahidi kutafuta kazi ili kugharamia mahitaji ya familia. Anamchukulia Mumbo kuwa mwongo anaposema kuwa anajitahidi kutafuta kazi, kuuandika mswada na kutafuta mchapishaji. Mtazamo huu wa mke wa Mumbo unaisambaratisha ndoa yao.

Mkewe Mumbo anamdharau na kumdunisha mumewe kwa kutoyamudu mahitaji ya familia. Mumbo anasema,

> "Mke wangu ananiita mzembe, mbona siwezi kupata kazi kama wanaume wengine, wana nini ambacho sina. Ni mwanamume mgani ambaye siwezi kukidhi jamaa yangu? Kwani ni mwanaume suruali tu. Na hata hiyo suruali ni heri niivue nijiendee uchi?" (uk. 158).

Kumdunisha huku ni kumdhulumu kisaikolojia na kumpokonya mamlaka yake kama mume na kwa hivyo kusambaratisha ndoa yao.

Siku moja wanapojibizana baada ya watoto kufukuzwa shuleni kwa karo, mkewe Mumbo anauchukua mswada ambao Mumbo ameurekebisha na kuutupa nje ambako unaharibiwa na maji ya mvua. Huu ni ukatili na dhuluma kwa mume wake kwa sababu hajali kazi ambayo mume wake ameifanya kuuandika, kuurekebisha na kutafuta mchapishaji. Pia,

hajali kuwa mswada huu ndio tumaini la pekee la mumewe kujipa fedha. Mumbo anachelewa kuupeleka kwa wachapishaji na kwa hivyo hauchapishwi. Kitendo hiki cha mkewe Mumbo kinasambaratishasha uhusiano wake na mumewe na hali kadhalika ndoa yao.

Anapofahamu kuwa mswada umekataliwa, mke wa Mumbo anamcheka mumewe kisha anamtoroka. Anawatorosha watoto wao pia. Huu ni ukatili na dhuluma kwa mume wake kwa sababu Mumbo ana haki ya kuishi na watoto wake au kupata fursa ya kuwaona. Kwa kumkimbia Mumbo, mke wake anaisambaratisha ndoa yao.

**2.8.0 DAPHINA NA AMI YA MUMBO**

Daphina ni mke wa ami ya Mumbo. Si mengi juu ya ndoa yao yamesimuliwa isipokuwa tukio moja ambalo lilimwathiri Mumbo. Hakuna lolote lililosemwa juu ya ami ya Mumbo na kwa hivyo ni vigumu kutathmini uhusika wake katika ndoa yake.

**2.8.1 MCHANGO WA DAPHINA KATIKA NDOA YAKE**

Mumbo anawafumania Daphina na Kasu, rafiki yake mume wa Daphina, katika ugoni. Daphina anajaribu kumfanya Mumbo asifichue siri hiyo kwa kumkaribisha jikoni na kumpa nyama za kukaangwa. Tendo hilo la Daphina na Kasu halikubaliwi na jamii na ndio sababu walienda kujificha kichakani, na Daphina akamhonga Mumo asifichue. Kushiriki katika uzinzi kwa Daphina kunadhoofisha ndoa yake.

Baada ya muda fulani, Daphina anaondoka na kumwacha mumewe. Hapa anachangia kusambaratika na pengine kuvunjika kwa ndoa yao.

### 2.9.0 PASTA NA MKE WAKE

Pasta (mhubiri) na mkewe wana watoto watatu, mmoja wao akiwa Kaminda. Anaongoza ibada za kikristo kijijini kwao na hata ndiye anayeongoza ibada ya ndoa ya mheshimiwa Kaa-sisi (Kasina) na mke wake wa tatu.

### 2.9.1 MCHANGO WA PASTA KATIKA NDOA YAKE

Mumbo anamshuhudia Pasta akishiriki katika uzinzi na mke wa mzee wa kanisa usiku mmoja wakati wa ibada ya kuukaribisha mwaka mpya (uk. 149-159). Kitendo hiki kinaisambaratisha ndoa yake kwa sababu ni usaliti kwa mke wake. Pia, Pasta anajitokeza kama mnafiki kwa ajili anatenda kinyume na yale anayohubiri.

Mukini, mtoto wa pili wa Pasta na mkewe, anatoweka nyumbani kwa sababu "…hapendi kumwona mamake anayeishi maisha ya kimya: kwamba kila alisemalo mumewe anaitikia na hafungui kinywa chake kupinga lolote" (uk. 163). Anaashiria kuwa Pasta anatawaliwa na itikadi ya kiubabedume ambapo mwanamke hana nafasi ya kutoa maoni yake katika ndoa. Kwa sababu hii, Pasta anasambaratisha ndoa yake.

### 2.9.2 MCHANGO WA MKE WA PASTA KATIKA NDOA YAKE

Si mengi yameelezwa juu ya mke wa Pasta isipokuwa kwamba ni mnyamavu, hajadiliani na mume wake wala haping lolote. Anachangia kuisambaratisha ndoa yake kwa sababu hatoi maoni ambayo yanaweza kuiimarisha zaidi. Pia, yawezekana kuwa ana ufahamu wa maovu ambayo mumewe anatenda lakini amenyimwa sauti ya kuyapinga na kwa hivyo, Pasta anaendelea na tabia zake mbovu.

### 2.10.0 KAMINDA MWANA' A PASTA NA SASI

Kaminda mwana'a pasta ni kijana mwadilifu anayezingatia mahubiri ya baba yake, kinyume na watoto wengine wa wahubiri, wakiwemo ndugu zake wawili. Hata anapoendelea na maisha yake mjini, hana nia ya kuoa, ana mawazo changamano kuhusu ndoa.

> "…alikuwa bado kapera wala hata hajawazia jinsi ya kuuasi ukapera huo, au kwa maneno ya Waswahili, kupata jiko (la kuchoma au kupasha moto hajui) (uk.164).

Hata hivyo, mtazamo huu wake Kaminda unabadilika polepole Sasi anapoanza kuishi naye, na baada ya mwaka mmoja, wanafunga ndoa. Wanajaliwa watoto watatu. Ndoa yao inaanza kutingisika baada ya Kaminda kugundua kuwa msichana anayedhani ni wa dada ya Sasi alikuwa mwanake Sasi. Ndoa yao inavunjika siku moja Sasi anapomtisha kumwua.

### 2.10.1 MCHANGO WA KAMINDA KATIKA NDOA YAKE

Baada ya kugundua kuwa Sasi hana nia ya kutafuta nyumba yake na uhusiano wao umestawi kiasi ni vigumu kuwatengenisha, Kaminda anaamua kumjulisha baba yake ili wahalalishe uhusiano wao. Wanafunga ndoa. Kwa kumfahamisha baba yake, juu ya uhusiano wao, Kaminda anastawisha ndoa yake kwa sababu anataka itambulike kulingana na sheria za nchi.

Mwanzoni mwa ndoa yao, Kaminda anaanza kumwamini Sasi na hata kujilaumu kwa mashaka aliyokuwa nayo. Imani hii inapelekea kunawiri kwa ndoa yao.

Kaminda ana uhusiano mzuri na nyanya na babu ya Sasi. Anaandamana na Sasi kuwatembelea mara kwa mara. Pia, anajitolea kumwelimisha msichana anayeambiwa ni wa marehemu dada yake Sasi, na kila anapoenda katika soko la mtumba anamnunulia nguo. Huu ni utu wema unaostawisha ndoa yao.

Kaminda ni mtu mpole ambaye hasemi ovyo hata akiwa na hasira. Hutafakari kabla ya kunena. Mfano ni anapogundua kuwa msichana anayeambiwa ni wa dada yake Sasi ni mtoto wake Sasi, anapofika nyumbani hasemi lolote na anapomwambia Sasi, anamwambia kwa upole. Sifa hii yake inachangia pakubwa kustawisha ndoa yao kwa sababu Sasi ana tabia ya kuongea kabla ya kutafakari na kuongea sana.

Kaminda ameshika vyema imani ambayo amefundishwa na wazazi wake. Jambo moja alilofundishwa ni kuwa ndoa zinatoka mbinguni na kwa hivyo, hazifai kuvunjwa ovyo ovyo. Kwa sababu hii, anamsamehe Sasi kwa kutomwambia ukweli. Msamaha katika ndoa hurejesha uhusiano mwema, na kuiimarisha ndoa.

Kwa kutaka kumjua Sasi vyema zaidi, Kaminda anafanya uchunguzi. Anapata habari, chungu nzima ambazo anataka Sasi amthibitishie. Hizi ni juhudi za kustawisha ndoa yake kwa sababu anasaka ukweli.

### 2.10.2 MCHANGO WA SASI KATIKA NDOA YAKE

Sasi anamyemelea Kaminda akiwa na nia moja, kulipiza kisasi kwa mtoto wa Pasta kwa sababu mchumba aliyemtelekeza alikuwa mtoto wa Pasta. Anamfanyia Kaminda hila na mwishowe, Kaminda anamuoa. Hila hii inafichuka miaka mingi baadaye na Kaminda anapomwuliza, mtafaruku unazuka, na kwa hivyo, Sasi anaisambaratisha ndoa yake zaidi.

Sasi ni mdanganyifu. Anamdanganya Kaminda kuwa anahitaji kusaidiwa na mahali pa kukaa akitafuta nyumba. Pia, anashirikiana na nyanya yake kumdanganya Kaminda kwamba yule msichana ni mtoto wa dada yake Sasi. Baada ya Kaminda kugundua ukweli, anapatwa na uchungu. Mawasiliano yao si mazuri kwa sababu Sasi anakasirika sana na kumshtumu Kaminda. Uhusiano wao unazorota.

> "Usiku huo, kwa mara ya kwanza katika maisha yao, kila mmoja alijifunika blanketi lake. Na si hilo. Walionyeshana migongo; kila mmoja amejikunja na kuunda uta wa masikitiko…wote wanapumua kwa nguvu kama watu waliotenganishwa kabla ya kuvaana, hasira bado inafoka kama chungu cha maboga, Mbegu mbaya ikawa imeatikwa kati yao. Maongezi yao kila wakati kuanzia siku hiyo yakawa ni nyama iliyotumbukia nyongo. Jambo dogo tu, Sasi

> anaruka na "Ulikuwa unanichunga!" (uk.173).

Kaminda anaamua kufanya uchunguzi zaidi na anagundua mambo mengi zaidi ambayo yanamwudhi Sasi zaidi anapoulizwa.

Sasi hamwamini Kaminda tena baada ya mapenzi yao kuanza kufifia. Anamshuku Kaminda kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na wanawake wengine.

> "Mkewe Sasi akawa anamshuku kila wakati. Akichelewa kidogo nyumbani ni kwa sababu amevutiwa na wanawake wa mtaani. Akimwona anacheza na watoto wa jirani ni kwa sababu anataka kuwafurahisha mama zao. Akinyamaza kama ilivyo tabia yake, ni kuwa amenyamazia na si kwa nia nzuri bali ni mbaya." (uk. 168).

Kuna tatizo la mawasiliano ambalo linaendelezwa na Sasi kwa kumshuku na kutomwamini mume wake. Kwa hivyo anaisambaratisha ndoa yake.

Sasi hataki jamaa za Kaminda waishi nao kwa sababu ana hofu kuwa watamchunguza ilhali anawaalika jamaa zake kuishi nao wakati Kaminda anapokuwa kimya. Tabia hii ya

Sasi inachangia kusambaratika kwa ndoa yao kwa sababu Kaminda anaanza kuwa na shaka juu yake.

Sifa hasi ya kutomheshimu mume inadhilirika anapomtusi Kaminda akitumia "maneno yote ya matusi aliyoyajua" (uk. 174) baada ya Kaminda kumwuliza juu ya mambo anayoyagundua katika uchunguzi wake. Kutomheshimu mume husambaratisha ndoa.

Ukatili na dhuluma zinadhihirika katika Sasi anapogunduliwa kuwa kwenda kwa Kaminda si kuomba mahali pa kujisetiri bali kulipiza kisasi ilhali si Kaminda aliyemkosea. Pia, sifa hizi zinadhihirika Sasi anapojaribu kumwua Kaminda kwa kisu. Kitendo hiki kinapelekea kuvunjika kwa ndoa yao kwa sababu Kaminda anajinasua na kutoroka kabisa.

**2.11.0 KASSIM NA WAKE ZAKE**

Kassim (Wamae) anatoka kwa jamaa fukara wanaoishi maisha ya uchochole na kwa hivyo anashindwa kuendeleza masomo yake baada ya kumaliza masomo ya sekondari. Anajaribu kutafuta msaada kutoka kwa mbunge wao bila kufanikiwa. Anaanza biashara ndogo kwa kukopa mtaji. Biashara zake zinaendelea kupanuka na anakuwa mwanabiashara mashuhuri. Pia, ni mwananchi mwenye nia njema kwa sababu anawasaidia wanakijiji kwa kutoa msaada wa fedha kufidia elimu. Kassim ana wake wawili. Ni machache mno yameelezwa kuhusu mke wake wa kwanza.

### 2.11.1 KASSIM NA MKE WA KWANZA

Si mengi yameandikwa kuhusu uhusiano wa Kassim na mkewe wa kwanza ila kuwa hakuwa anamfichulia siri nyingi kama vile anavyomfichulia Betty, mkewe wa pili. Kassim hamwamini mkewe wa kwanza; na kutomwamini kunaisambaratisha uhusiano wao na hali kadhalika, ndoa yao.

Kassim anamuoa mfanyi kazi wake, Betty. Anadhoofisha uhusiano wake na mke wake wa kwanza.

Baada ya Kassim kutupwa katika gereza kuu, mke wake wa kwanza anatorokea kwao na watoto wao kwa kutopatana na hali ilivyo. Kulingana na desturi za Kiafrika, kurudi kwao ni kuukata uhusiano na mumewe na kwa hivyo, anaisambaratisha ndoa yake.

### 2.11.2 KASSIM NA BETTY

Betty ni mfanyikazi wa za Kassim, na Kassim anamwoa baada ya muda fulani. Kassim anamwamini sana, kiasi cha kumfichulia siri nyingi ambazo mke wake wa kwanza hazijui (uk.192). Kwa Kassim, kumfichulia Betty siri nyingi ni kuiimarisha ndoa yao.

Baadaye, uhusiano wao unafifia na Kassim anaadimika nyumbani mwao, jambo ambalo halimpendezi Betty, na anaenda kutafuta ushauri nasaha kutoka kwa Dr Thetis. Kutafuta ushauri nasaha ni juhudi dhahiri ya kuzuia ndoa yake kusambaratika.

Kutokana na uchunguzi wa Dr Thetis, inaonekana kuwa mawasiliano baina ya Betty na Kassim yamefifia. Kulingana na Dr Thetis, mawasiliano duni husambaratisha nyanja

nyingine zote za ndoa yao na ndipo wana tatizo la *conjugal impotence*. (uk. 187-188). Kassim anaonekana kutoshiriki kikamilifu kimawasaliano na kwa hivyo anasaimbaratisha ndoa yao.

Betty anapotambua kuwa kuna matatizo katika ndoa yao, anaenda kutafuta suluhisho peke yake. Inaashiriwa kuwa alimwambia Kassim waandamane lakini Kassim anakataa:

> "...Mwenyewe Kassim alisema hakuwa na wakati wa kwenda kumsikiliza mtu akimweleza jinsi ya kuishi." (uk.187)

Kassim anaizorotesha ndoa yake kwa kutotafuta suluhisho la matatizo baina yake na mkewe.

Baada ya himaya ya Kassim kuporomoka ndipo anagundua kuwa Betty, mke wake aliyemwamini sana na kumfichulia siri nyingi za biashara yake, ndiye alikuwa katibu muhtasi wa zamani.Kuna uwezekano kuwa Betty akija kwa Kassim nia yake haikuwa kumfanyia Kassim kazi, bali kumchunguza Kassim, kuzijua siri zake na kisha kumpelekea Mbunge Atiriri habari hizo ili amwangamize Kassim, asipate fursa ya kumpinga katika kuwania kiti cha ubunge. Yawezekana pia, Betty anaolewa na Kassim Betty atimize maagizo ya Mbunge Atiriri na kwa sababu hii, anaizorotesha ndoa yake.

### 2.12.0 SIR PIPO NA LULU.

Sir Pipo anaanza urafiki wake na Lulu akiwa chuo kikuu naye Lulu akiwa mwalimu wa shule ya sekondari ambaye hajapata mafunzo ya ualimu.

Pipo anamsaidia Lulu kwa mambo mengi kama vile kugharamia matibabu ya nyanya yake, kumtafutia nafasi ya kusoma katika chuo cha ualimu, kugharamia mahitaji ya kibinasfi ya Lulu, kumpa moyo kusomea shahada ya digrii ya kwanza ya ualimu na kumtafutia mfadhili wa shahada ya pili. Lulu anapokuwa akisoma shahada ya pili ndipo wanaamua kufunga ndoa.

### 2.12.1 MCHANGO WA SIR PIPO KATIKA NDOA YAKE

Sir Pipo anataka kuwa na ndoa inayotambulika rasmi ndipo anatuma ujumbe kwa jamaa za Lulu kuwa atakwenda kumposa. Wanapokwenda kwa jamaa za Lulu na kuitishwa mahari nyingi, Pipo anampendekezea Lulu waende kwa mkuu wa Wilaya na kufungia ndoa yao huko, jambo linalopingwa na Lulu. Pipo anajitahidi kupata pesa za kulipia mahari ili aweze kumwoa Lulu kirasmi. Hii ni juhudi ya kuiimarisha ndoa yake.

Baada ya Pipo na Lulu kufunga ndoa, Pipo anaanzisha biashara kadhaa ili kufidia fedha alizotumia kulipia mahari. Hii ni juhudi dhahiri ya kuiimarisha ndoa yake kwa sababu hataki wapungukiwe.

Lulu anapokataa kula chakula cha kawaida ili apunguze unene wake, Pipo anatafuta ushauri wa wataalamu na kumnasihi Lulu ipasavyo kwa sababu hataki mke wake ajidhuru. Anajitahidi kuistawisha na kuitunza ndoa yake.

Kwa kuwa hataki mtafaruku katika ndoa yake, Pipo anazingatia ushauri wa rafiki yake na kutomwuliza Lulu lolote anapoanza kumeza vidonge vya kusafisha uto wote mwilini na kuwa na umbo la kuvutia. (uk. 208). Pipo anataka ndoa yake iwe na amani na hali kadhalika iimarike.

Lulu anapojiunga na kikundi cha marafiki zake ili kuinuana kiuchumi, Pipo anamsaidia kupata mtaji ambao ni mkubwa. Hii ni juhudi ya kuwa na uhusiano mwema na kumpa Lulu fursa ya kujiendeleza kiuchumi.

Pipo anajitahidi kuwasiliana na mke wake juu ya masuala muhimu kuhusu ndoa yao, mifano ni suala la kupata mtoto na swala la kuadimika nyumbani (uk. 209).

Kutokana na malalamiko ya Lulu, Pipo aliutumia wakati wake mwingi katika kuchuma mali:

> "…na mumewe ambaye alikuwa amepandwa na pepo wa mali ambaye hakumruhusu kutulia hata akiwa kitandani." (uk 209)

Maneno “Pipo kutotulia hata akiwa kitandani” yaashiria kuwa mahusiano ya Pipo na Lulu kama mume na mke hayamridhishi Lulu. Kwa kuzama sana katika biashara zake, Pipo anasambaratisha ndoa yake kwa sababu hampi mke wake wakati wa kutosha.

### 2.12.2 MCHANGO WA LULU KATIKA NDOA YAKE

Baada ya kufunga ndoa, Pipo anajizatiti kuanzisha biashara kadhaa ili kufidia fedha alizotumia kumlipia Lulu mahari. Jambo hili halimpendezi Lulu.

Maoni ya Lulu kuwa “amegeuzwa mtu wa kumtegemea mume tu kama vijana wanaotoka kutegea kumbikumbi wakati wa mvua” (uk 209) yanaisambaratisha ndoa yake kwa sababu hazitambui juhudi za mume wake.

Lulu anakataa kuzingatia ushauri wa wataalamu wa lishe ambao Pipo anaenda kwao kupata ushauri kuhusu unywaji wa sharubati ya karoti pekee ili kupunguza unene. Licha ya hivyo, anaanza kumeza vidonge vya kusafisha uto mwilini. Kwa kutojali afya yake na kukataa kuzingatia maoni ya mume wake, Lulu anaisambaratisha ndoa yake. Kwa maneno ya msimulizi, “wakaanza kuvutana kwa mambo madogo.” (uk 208)

Baada ya Lulu kujiunga na rafiki zake ili kujiendeleza kiuchumi, panazuka mtafaruku baina yake na mume wake, aliyemsaidia kwa fedha za kuanzia mradi huo. Wanazozana kwa sababu Lulu sasa hana wakati wa kutulia nyumbani, anasafiri na wenzake hata nje ya nchi ili kuboresha biashara zao. Lulu anaisambaratisha ndoa yake kwa kumwacha Pipo katika upweke.

Lulu anajikita katika utafiti wa ufeministi wa kiharakati ambao una athari katika mwona ulimwengu wake. Lugha yake inayojitokeza katika usemi taarifa na usemi halisi inadhihirisha rai hii;

> "…anataka mwanda wa kujishasha kama kiumbe….Akalalamika hali ya kugeuzwa pambo tu nyumbani na mumewe…. Akachukizwa na wivu wa mumewe usiokuwa na sababu na nia yake ya kumliki kama chombo…."Pipo umenioa tu, hujanimiliki!" akalalamika siku moja. (uk 209).

Lulu anaisambaratisha ndoa yake kwa kushikilia misimamo ya wanaharakati wa ufeministi wa mrengo huu ambao wanapendekeza wanawake wasiolewe (Greer: 1970). Hatimaye, anasema anataka uhuru wake ili aendeleze shughuli zake, "bila kubughudhiwa na kinywa cha mwanamume" (uk. 210).

Lulu hana heshima katika mawasiliano na mumewe, pamoja na kummnyima hadhi yake kama mume. Anamwambia kuwa amemuoa tu wala si kummiliki, Pipo anataka kumidhibiti kama chombo na shinikizo la kupata mtoto linatoka kwake Pipo au mama yake (Uk. 209). Kutumia lugha yenye makali na kutomheshimu mume wake ni dhuluma

dhidi ya mumewe pamoja na kudhoofisha mawasiliano baina yao wawili, na hali kadhalika kuisambaratisha ndoa yao.

Kwa kukataa kumpata mtoto, Lulu anamdhulumu mume wake kwa sababu ya kumnyima haki yake ya kuwa mzazi. Pia, anatekeleza dhuluma dhidi ya mumewe kwa kummithilisha na babake, ingawa kimoyomoyo (uk. 211). Kulingana na Munavi (1988:158), huo ni ushari usio wa moja kwa moja. Dhuluma hizi zinasambaratisha ndoa yao.

Kikundi ambacho Lulu anajiunga nacho kina athari kubwa katika mienendo yake. Anataka kuwa huru kama wenzake wengine wote. Hatimaye, wanaachana na ndoa yao kuvunjika.

**2.13.0 PURUPESA NA TRUVESSA**

Purupesa na yatima anayelelewa katika makao ya watoto baada ya kifo cha mama yake punde tu, anapomzaa.

Purupesa si jina lake kutoka utotoni lakini ni lakabu aliyopewa na mwanamke mwenda wazimu aliyesema. “Huyo atakuwa Purupesa siku moja” (uk. 216)

Baada ya Purupesa kufika kilele cha masomo na kufanya kazi kwa muda, ndipo anagundua kuwa kuna ombwe katika maisha yake; hana mke. Anamuoa Truvessa, mwanafunzi wake wa zamani, ambaye ni mdogo wake kwa miaka kumi na mitano.

### 2.13.1 MCHANGO WA PURUPESA KATIKA NDOA YAKE

Mahusiano ya Purupesa na mke wake yameathirika kwa Purupesa kutolewa tezi-shahawa inayoelekea kuwa chanzo cha saratani. Mahusiano yao yanazoroteshwa zaidi na fikra kuwa, kutolewa tezi-shahawa ni sawa na kuhasiwa, na kumbukumbu za jinsi anavyodhulumiwa kimapenzi akiwa mtoto. Purupesa hatafuti ushauri wa daktari na wataalamu wa kisaikolojia ili aweze kukabiliana na changamoto hizi ambazo zinazorotesha ndoa yake.

Purupesa anachangia kuzorota kwa mahusiano baina yake na mke wake kwa kusoma sana katika maktaba yake ili kukabiliana na upweke. Ingawa inaonekana kuwa njia ya kisaikolojia ya kuilinda nafsi yake. Mkewe analalamika (uk. 222) na pia, anavichoma baadhi ya vitabu vyake.

Purupesa hamwambii Truvessa mambo yanayomsumbua kibinafsi kama vile, dhuluma aliyofanyiwa akiwa mtoto na aliyoyasikia kuhusu kutolewa tezi-shahawa. Hapana mawasiliano katika uwanja huu muhimu wa ndoa yao, na kwa hivyo anaisambaratisha ndoa yake.

Purupesa anajitahidi kuwasiliana na mkewe kuhusu mambo yanayomchukiza katika ndoa yao. Mfano ni Truvessa aliporudi nyumbani kutoka *Avocado Wasp*. Kwa kuwasiliana na mkewe juu ya masuala muhimu katika ndoa yao, anatia juhudi kuiimarisha ndoa yao.

Purupesa ni mwepesi wa kumsamehe mke wake. Anamsamehe Truvessa anapouchanachana mswada wa kitabu chake na baada ya ghasia ya kumfumania *Avocado Wasp*. Vilevile anaenda kumliwaza Truvessa hospitalini ambako amelazwa ingawa ameshamtelekeza Purupesa. Kumsamehe Truvessa kunarejesha utulivu katika ndoa yao na kwa hivyo kuistawisha.

### 2.13.2 MCHANGO WA TRUVESSA KATIKA NDOA YAKE

Baina ya Truvessa na Purupesa mna tofauti ya miaka kumi na mitano. Yawezekana Truvessa anataka mume ambaye angemwezesha kuishi "…kama kijana wa siku hizi." (uk 220).Pia, anasema kuwa aliolewa "...na mwanamume amtunze yeye…."(uk.221)

Mahusiano ya Purupesa na Truvessa yanapodhoofika, Truvessa anahisi kuwa yanasababishwa na tatizo fulani alilo nalo mume wake. Kosa analofanya ni kuwa hajadiliani na Purupesa juu ya suala hili nyeti bali anamfichulia rafiki yake Lulu.
Licha ya hayo, anapuuza pendekezo la Lulu la kuchunguza ikiwa Purupesa anaathiriwa na tukio ambalo laweza kuwa lilitokea akiwa mtoto (uk 221). Hapa, anasisambaratisha ndoa yake pakubwa kwa sababu maswala yanayoathiri mahusiano yao kama mume na mke ni ya kisaikolojia.

Purupesa anatumia muda wake mwingi katika vitabu na kuandika mswada kama njia ya kisaikolojia kufidia udhaifu wake, Truvessa anadhani kuwa anampuuza. Analipiza kisasi kwa kuvichoma baadhi ya vitabu vya Purupesa na kuuchanachana mswada wake. Hii ni dhuluma kwa mumewe na kwa hivyo anaisambaratisha ndoa yake.

Truvessa ni mwongo. Anamdanganya mume wake kuwa ana miadi na rafiki yake ilhali anaenda *Avocado Wasp* kuwachezea wateja densi ya nusu uchi na kuvua nguo.Uongo huu unaidhoofisha ndoa yao hasa, baada ya Purupesa kugundua ukweli. Wanagombana kwa muda na kwa hivyo hakuna amani katika kipindi hiki.

Truvessa anaenda *Avocado Wasp* kucheza densi akiwa nusu uchi ili kuwatia wateja ashiki na kuwafurahisha ili watoe pesa. Kulingana na fasili za Weitzer (2000:1-10) na Amissah (2005:3-4), kahaba ni mwanamke anayeshiriki katika ngono au katika vitendo vinavyotia ashiki kama vile uchezaji densi nusu uchi na kuvua nguo, mazungumzo na ugusaji unaotia ashiki kwa minajili ya kupata fedha, mihadarati au vitu vingine vya thamani. Kwa hivyo, Truvessa ni kahaba. Baada ya Purupesa kugundua sifa hii ya Truvessa, anachukizwa sana na mtafaruku mkubwa unazuka baina yao.

Inadhihirika kuwa Truvessa amejiunga na wanaharakati wa ufeministi. Kwanza, ni kuwa ni rafiki ya Lulu ambaye anazingatia ufeministi wa kiharakati. Wanapogombana anatumia semi zinazoonyesha mwono ulimwengu wake mifano ni.

> "…Nataka uhuru wa kujieleza na kuyaishi mawazo yangu. Napenda kuizifurahia njozi zangu bila ya kuzuiliwa na matarajio ya asasi kama ndoa au utamaduni.
>
> Uhuru hauna aibu. Kwa nini niyabanie mawazo yangu ndani yachipukizie kwenye

> ndoto tu kwa jamii iliyotiwa pingu na mila imeyakataza?...Rafiki yangu Kamene alimwoa mtu aliyesoma akidhani mtazamo wake ni tofauti kumbe ni ule ule?…Mambo yamebadilika siku hizi Profesa…hata watu wanaenda *Swinger Clubs* wanakobadilishana wake au waume ili kutia iliki kwenye mahusiano yao yaliyokosa ladha. Ukale hauna nafasi tena katika maisha yetu!" (uk. 232-233).

Ufeministi wa kiharakati unapinga asasi ya ndoa kwa hivyo, Truvessa anaisambaratisha ndoa yake kwa kuzingatia mienendo ya ufeministi huu.

Truvessa anamwacha Purupesa na inaonekana kutoka kwa ujumbe anaouacha ni kwa sababu kuna jambo fulani ambalo Purupesa anashindwa kutekeleza, kutokana na athari ya hitilafu inayotokea anapofanyiwa upasuaji mara ya pili. Huu ni ukatili kwa sababu si mapenzi yake Purupesa kutotimiza jukumu hilo. Kwa Truvessa kumtelekeza Purupesa, anasambaratisha ndoa yao kabisa, hawaishi tena kama mume na mke.

### 2.14.0 KASINA USINA NA WAKE ZAKE

Mheshimiwa Kasina Usina Sini amefuata mkondo wa wanaume wa ukoo wao wa kutotosheka na mke mmoja. Yeye ana wake watatu. Kwanza anawaoa wawili kwa

kuzingatia mila na desturi na hatimaye, anamwoa mke wa tatu kwa kufunga ndoa kanisani.

### 2.14.1 MCHANGO WA KASINA KATIKA NDOA ZAKE

Kasina anaonekana kuwa anawaoa wake zake sio kutokana na mapenzi, lakini ili kukidhi mahitaji fulani. Anawaoa wake wawili wa kwanza ili kufuata nyayo za baba na babu yake, yaani kuwa na zaidi ya mke mmoja na kwa hivyo kuwafurahisha (uk. 239). Anamuoa mke wa tatu, Tina Yaipan, baada ya kuchaguliwa kuwa mbunge. Anamtaka mke "...wa kisasa anayeweza kwenda na wakati na kuwakaribisha wageni wa ngazi ya juu" (uk. 246).

Kasina hampi mke wake fursa ya kupumzika ili aweze kufurahia mahusiano yao ya mume na mke. Jambo hili linafanya mkewe kurudi kwao na kulalamika. Ingawa mkewe anarudi kwa mumewe, haifurahii ndoa yake (uk. 239). Hapa, Kasina anaisambaratisha ndoa yake.

Kwa kuwa hatosheki na mahusiano na wake zake, Kasina anakuwa na mahusiano na wanawake wengine wakiwemo vijakazi waliomo nyumbani mwake. Anapata watoto na wanawake hawa (uk. 239-247). Anashiriki katika uzinzi ambao unazorotesha ndoa zake. Wake zake wanachukizwa na jambo hili (uk. 240, 241).

Anapomshuku mkewe kuwa ana uhusiano nje ya ndoa, hawasiliani naye kuhusu suala hili bali anaenda kupata ushauri kwa baba yake. Matokeo ni kuwa wakeze wanaibika

katika sherehe inayoandaliwa na Mzee Usina, na wanamshuku mume wao kuwa amekula njama na baba yake na mganga. Wanatamani kujilipizia kisasi (uk. 245). Kutowasiliana na mke wake kunazorotesha ndoa zake.

Katika uk. 247 tunaarifiwa kuwa Kasina anataka kumwacha Maria, mkewe wa pili, hasa kwa kuwa hana mtoto. Kasina anaisambaratisha ndoa yake na Maria kwa kuwa hafuatilii kujua tatizo liko wapi.

Hatimaye, Maria anajaliwa kushika mimba. Wakati wake wa kujifungua unapofika, anaumwa nyumbani kwa siku nzima kisha kupelekwa hospitali kwa gari la serikali. Lakini, kwa kuolewa akiwa mchanga, kutahiriwa na kwa maumivu ya kujifungua kwa muda mrefu, anapata tatizo la *Obstetric Fistula*. Kama Kasina angekuwepo Maria anapoanza kupata uchungu, au angekuwa amepanga mpango wa kumpeleka hospitali, haya hayangetokea. Kwa hivyo, anaisambaratisha ndoa yake.

Kasina anamtelekeza Maria kwa kuwa ana hofu ya kuambukizwa ugonjwa alio na Maria (uk. 249). Hata Maria anapokuwa hospitalini kurekebishwa hitilafu hii, Kasina hamkaribii. Kwa kumtelekeza mkewe, Kasina anaisambaratisha kabisa ndoa yake.

Hata hivyo, Kasina ana sifa chanya zinazoiboresha ndoa yake. Anawapa wake zake mahitaji yao yote ya kimsingi. Hii inadhihirika wanapolalamika, naye haoni sababu yao kulalamika.

> "…wakeze walipolalamika akawa anawaaambia kuwa wana kila kitu wanachokitaka. Kwa nini wamsumbue? Wake wengine wanalilia kupata nusu ya nafasi waliyokuwa nayo."Pia, baada ya kuwachaguliwa mbunge, anamwachia mke wa kwanza duka lake. (uk241)

Ingawa Kasina hataki kumkaribia Maria kwa ajili ya hitilafu aliyopata akijifungua, anatoa fedha za kugharamia matibabu. Hapa anawajibika na kwa hivyo kuistawisha ndoa yake na Maria.

**2.14.2 MCHANGO WA WAKE ZA KASINA**

Mke mmoja wa Kasina ameudhiwa na ukware wa mumewe. Baada ya kushindwa kumzuia, anatafuta msaada kutoka kwa mganga. Hata hivyo, dawa aliyopewa haisaidii kamwe. Anaisambaratisha ndoa yake kwa kuwa uganga hausaidii.

Kutokana na tukio la Mzee Usina kutaka kumfunza mwanaye kuwa kuna wanawake wengi ambao si waminifu, na haipasi kumtaliki mke kwa sababu hii, inadhihirika kuwa bibi zake wameshakuwa na mahusiano na wanaume wengine nje ya ndoa. Kwa kutokuwa waaminifu, wanazisambaratisha ndoa zao, hasa ya Maria. Kasina anaamini kuwa Maria amepata *Obstetric Fistula* kwa kutokuwa mwaminifu na kwa hivyo anamtenga na kumwoa Tina Yaipan (Uk.249).

Wake wawili wa kwanza wa Kasina wanakasirika kwa kuaibishwa mbele ya watu na Kasina. Wanadhamiria kulipiza kisasi (uk. 245). Inaonekana wanalipiza kisasi kwa kuwakusanya watoto wote wa Kasina na mama zao ili Kasina atekeleze wajibu wake na kumuaibisha. Msimulizi anasema:

> "Wakati mheshimiwa Kasisi anapambana na hali hii, wakeze wawili…walikuwa wanamwangalia kwa mbali kisha kuangaliana kama wale Waarabu wa Pemba husemwa hujuana kwa vilemba. Kama wawindaji wawili wanaowaongoza mbwa wanaomzingira sungura kila upande akose la kufanya au mtu aliyemmulika mnyama kwa kurunzi usiku wa giza ashindwe kukimbia." (uk. 254)

Kisa kinamalizika kabla ya kueleza matokeo ya tukio hili lakini yaelekea ni mazito kwani kuna kijana anayetokea nyuma ya Kasina, pengine anamdhuru.

**2.15 HITIMISHO**

Katika sura hii, tumezichunguza ndoa zinazojadiliwa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* (2008) na kubainisha sababu zinazowafanya baadhi ya wahusika kufunga ndoa.

Tumechunguza kila mhusika katika ndoa yake na kutathmini mchango wake katika kuistawisha au kuisambaratisha ndoa yake. Tumegundua kuwa watu wa jinsia zote mbili wana uwezo wa ama kuziimarisha ndoa zao, au kuzisambaratisha kulingana na jinsi watakavyo kabiliana na changamoto zinazoikabili asasi hii. Kulingana na nadharia ya sosholojia ya fasihi riwaya hii imesawiri uhusiano na mivutano baina wake na waume wao katika jamii halisi (Swingewood 1975; Chalmers 1978;Wellek na Warren 1978; Kiiru 1978).

# SURA YA TATU

# CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI ASASI YA NDOA

## 3.0 UTANGULIZI

Katika sura ya pili, tumechanganua ndoa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* na kutathmini mchango wa kila mhusika katika ndoa yake. Baadhi ya vitendo vya wahusika vinasababishwa na changamoto zinazoikabili asasi ya ndoa na njia wanazotumia kukabili changamoto hizo zinazizorotesha ndoa zaidi. Pia, baadhi ya vitendo vya wahusika vinasababisha asasi ya ndoa kukabiliwa na changamoto nyingi.

Tashbihi na sitiari ambazo zimetumiwa katika riwaya hii zinadokeza kuwa asasi ya ndoa inakabiliwa na changamoto fulani. Nazo ni:

> "…ndoa ni kitu kama ule mchezo wa panya na paka; mzuri ukiwa paka lakini mbaya ukiwa panya." (uk 45)

> "Ndoa ni mchezo, walio nje wanatamani kuingia wacheze, na waulize watakwambia waingiapo watacheza vizuri kuliko waliomo ndani…." (uk. 49)

“ Maisha yao yakawa kama yule paka na panya wa runinga, *Tom and Jerry*, mkimbizano na kujifichaficha. ”

(uk. 69)

“…ndoa ni biashara ya hisi kati ya mwanamume na mwanamke.”

(uk. 165)

“...Ndoa kama safari ya maili mengi, inayoanza asubuhi wakati jua linatokeza mashariki, upepo mwanana unapigapiga na mioyo ina matumaini….”

(uk. 95).

“Ni kama mahindi yanayokuwa shambani asubuhi, yanayopigwa na upepo wa majira yale, na kuchezesha mabega yao kushangilia kwa matumaini makubwa.” (uk. 95).

“ Ndoa zote, kama ngano za fasihi simulizi zinaishia kwa ‘raha

mustarehe’ kisha zinafuatiwa na
mwanzo wa uhalisi wenyewe.”
(uk. 97)

Katika sura hii, tutazichanganua changamoto zinazoikabili asasi ya ndoa na kuisababisha isambaratike kama ilivyosawiriwa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*. Wataalamu wa masuala ya ndoa, Burleson na Denton (1997), Njue et al (2007), Chapman(2008) na Amulega et al (2009) wametafiti changamoto zinazoikabili asasi ya ndoa katika jamii ya karne ya 21. Tumezingatia nadharia ya soshojia ya fasihi na kulinganisha changamoto zinazoikabili asasi ya ndoa katika riwaya teule na zile zimetajwa na wataalamu hawa na hali kadhalika kuthibitisha kuwa huu ndio uhalisi uliopo katika jamii.

**3.1 UKATILI NA DHULUMA**

Azimio la Umoja wa Mataifa (1993) juu ya kumalizwa kwa dhuluma dhidi ya wanawake linafasiri dhuluma kama kitendo chochote ambacho huleta madhara, au kinaweza kuleta madhara ya kimwili, kimapenzi au kisaikolojia pamoja na vitisho vya vitendo hivi na kunyimwa uhuru kiholela au kwa kushurutishwa kufanya jambo au mambo pasina hiari. Chapman (2008:121-166) ameleeza jinsi dhuluma zilivyo katika ndoa. Anaeleza kuwa mamilioni ya wanawake na wanaume huathirika kila mwaka kutokana na ukatili na dhuluma katika ndoa.

Katika ndoa zinazosawiriwa na kujadiliwa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* changamoto ya dhuluma dhidi ya wake na waume inajitokeza. Kutokana na maneno ya wazazi wa

Kasekesi, inaonekana kuwa baba ya Kasekesi anamdhulumu mke wake. Mamake Kasekesi anamshauri bintiye amtafute mwanamume ambaye atamthamini kama kiumbe ingawa anatia shaka kuwa mwanamume kama huyo atapatikana. Inaonekana mumewe anamdhulumu kimapenzi kwa kuwa anasema:

> "Wanaume wa huku kwetu na mipini yao
> wanamchukulia mwanamke sawa na ardhi…
> ni kumbe wa kulimwa … ingelikuwa ni leo
> ningeliishi peke yangu…." (uk. 46)

Ushauri wa babake Kasekesi kwa binti yake unadhihirisha kuwa yeye ni mume anayemdhulumu mke wake kwa kushikilia mila za utamaduni uliopitwa na wakati. Anaamini kuwa mwanamume ndiye "kichwa cha nyumba" na anamsawiri mwanamume kama mwokozi wa mwanamke. Mfano ni katika semi zifuatazo:

> "…mwanamume ni kichwa cha nyumba. Kiwiliwili bila kichwa hakifai...mwanamke ni nguo, mgomba kupaliliwa…usiyasikilize maneno ya lipyoto wanaodai kuwa jamii yetu inamdharau mwanamke. Hasa mamao…mwanamume ndiye kiongozi wa nyumba na ndiye anayekufadhili katika maisha yako, anayekuongoza kwenye mapito ya giza katika ulimwengu huu

> katili, anayekueleza unapokwenda kombo, anakunasihi jinsi ya kuishi na wengine na uso wa kufadhiliwa u chini…mnyenyekee mumeo ili maisha yake yakunyokee….
> …wanaume wa huku kwetu wanamtunza mwanamke vizuri mradi usiwe na kichwa kigumu. Ukiadhibiwa kwa kuwa na utundu wa mkia wa nguruwe usirudi hapa!” (Uk. 47-48)

Agusto naye anamdhulumu Kasekesi kwa kuzua fujo anapokosa chakula ilhali anafahamu kuwa hali yao ya kiuchumi imezorota (uk. 54). Pia, kwa kuziiba fedha kidogo Kasekesi anazopata kutoka kwa biashara yake ili apate kukidhi uraibu wake wa pombe na kamari (Uk. 70). Agusto anamdhulumu Kasekesi kisaikolojia.

Kitonga anamlaumu Mwanamuka kwa kukosa kuzaa. Msimulizi anaeleza kuwa maisha yao yanakuwa kama vibonzo *Tom and Jerry* wa runinga wanaokimbizana na kutesana (uk. 69). Baada ya Mwanamuka kumwuliza mume wake kuhusu mimba ya kijakazi, mume wake anaanza kumtusi. Kuanzia hapo, mume wake anamwonyesha dharau nyingi, jambo linalomfanya Mwanamuka kuamua kutoka kwa ndoa hiyo. Kitonga anamdhulumu Mwanamuka kisaikolojia.

Baada ya Kamene kujifungua kwa njia ya upasuaji, Lusweti anamtesa kwa kumwacha nyumbani na mtoto pasina msaidizi. Lusweti anaporejea usiku wa manane, anatarajia

kuhudumiwa na Kamene bila ya kujali kuwa Kamene anaendelea kuuguza jeraha la kupasuliwa na ana mtoto mdogo anayehitaji kubembelezwa. Zaidi ya hayo, Lusweti anampiga Kamene kofi kwa kuwa Kamene amechelewa kumwandalia chakula (uk. 102). Lusweti anampiga mke wake mara ya pili kwa kumnyoa mtoto ilhali ni jukumu la mama mkwe (uk. 103). Ni dhahiri kuwa Lusweti amemdhulumu Kamene kimwili na, pia anamdhulumu kisaikolojia kwa kumnyamazia bila sababu (uk. 105). Anapomjibu Kamene kuwa mtoto atapona ikiwa ataweza kuhimili maradhi na ikiwa hatapona ni sawa (uk. 107) pia ni dhuluma ya kisaikolojia. Baada ya mahakama ya watoto kumwandikia Lusweti barua ili apate kuwajibika, anamtusi Kamene sana kwa lugha mbalimbali na kutishia kumtorosha mwanawe (uk. 107).

Mkewe Mumbo anamdhulumu Mumbo kisaikolojia kwa vitendo vyake. Kwanza, anamwita mzembe na kumdunisha kwa kushindwa kukidhi mahitaji ya familia yake (uk. 158). Pia, hatambui juhudi Mumbo anazotia kutafuta fedha, na anamzulia fujo. Anautupa mswada wa kitabu anachokiandika Mumbo kwenye mvua ambako unaharibiwa. Kwa sababu hii, inamchukua Mumbo muda mrefu kuusanifisha mswada lakini unakataliwa. Mke wa Mumbo anamcheka na kumtoroka na anawachukua watoto wao (uk. 160).

Sasi, anamtusi mumewe Kaminda anapoulizwa mambo fulani yanayohusu ndoa yao. Athari ya matusi haya inaonekana kwa vile Kaminda anashindwa na kula na kwenda chumbani. Kwa kiasi fulani, anamithilisha masaibu yake na ya Yesu (uk. 175). Sasi anamdhulumu mume wake kisaikolojia. Kaminda anazinduka kutoka usingizini na

kumkuta Sasi amemkalia tumboni huku ameshika kisu huku akihema. Ni dalili za Sasi kutaka kumwua Kaminda. Sasi anamdhulumu Kaminda kimwili na kisaikolojia.

Truvessa anadhani kuwa mumewe, Purupesa, anampuuza kwa kuwa anatumia wakati mwingi katika maktaba. Truvessa anavichoma nusu ya vitabu vilivyo katika maktaba ya kibinafsi ya Purupesa. Muda mfupi baadaye, anauchanachana mswada ambao Purupesa alikuwa ameuandika. Hatimaye, Truvessa anamtelekeza Purupesa kwa kuwa haridhiki na uhusiano wao. (uk. 234). Tukio hili linamwathiri Purupesa sana kwa kuwa anampenda Truvessa. Kwa jumla, Truvessa anamdhulumu Purupesa kisaikolojia kwa matendo yake.

Kutokana na usimulizi wa Kaseli Nzeli, Maria anaachishwa shule akiwa darasa la tano na kuozwa ndipo anapatwa na maradhi fulani (uk. 114). Maria anarejelewa katika uk. 239 wakati anarudi kwao kwa kuwa mumewe, Kasina, hampi nafasi ya kupumzika na kufurahia mahusiano yao (uk. 239).Aanamdhulumu mkewe kimapenzi. Baada ya Maria kupata jeraha katika sehemu za siri, kwa kutohudumiwa kwa muda ufaao wakati wa kujifungua, mume wake anamtelekeza na hali kadhalika, kumdhulumu kisaikolojia.

### 3.2 UKOSEFU WA MAWASILIANO BORA

Mawasiliano ni muhimu katika jamii kwa sababu yanahimili ushirikiano na hali kadhalika kuboresha uhusiano na maendeleo.Wataalamu wa masuala ya ndoa Burleson na Denten (1997: 884) wanasema kuwa mawasiliano ni wajibu muhimu katika ndoa. Tunachukulia kuwa ni jukumu la kila mwanandoa kuwasiliana vyema na mwenzake.

Baadhi ya ndoa zilizomo katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* zinakumbwa na changamoto za ukosefu wa mawasiliano bora na kwa hivyo, kusambaratika.

Ndoa ya Kasekesi na Agusto inakumbwa na changamoto ya ukosefu wa mawasiliano bora. Agusto hamwelezi Kasekesi undani wa safari zake, marafiki zake wala hali yao ya kiuchumi. Naye Kasekesi kwa kuzingatia nasaha ya baba yake, hamuulizi Agusto (uk. 50). Hata Kasekesi anapohisi pana jambo ambalo limeenda kombo, anashindwa atakavyomuuliza Agusto (uk. 52). Kwa kutofahamu mambo mengi kuhusu hali ya ndoa yao, ndipo Kasekesi anasema kuwa mume wake, alikuwa "mume wa giza" na ndoa yao "ndoa ya giza".

Kitonga ana ujumbe muhimu kwa mke wake, Mwanamuka, lakini anamtuma dada yake auwasilishe ujumbe huo (uk. 70). Kenzi anauwasilisha ujumbe na zaidi ya hayo anamtusi Mwanamuka. Mwanamuka anapomuuliza Kitonga kuhusu ule ujumbe, Kitonga anazua fujo. Ndoa yao inakabiliwa na changamoto ya mawasiliano mabaya.

Ndoa nyingine inayokabiliwa na changamoto ya mawasiliano mabaya ni ya Nyakor na mume wake. Wakiwa katika mazungumzo ya kupatana baada ya kipindi cha ubaridi katika ndoa yao, Nyakor anatoa kauli kwa lugha ya Kiingereza (uk. 79). Mumewe anazua fujo kwa kuwa anachukulia kuwa Nyakor anaidharau taalumu yake. Nyakor anajaribu kujieleza lakini mume wake hamwelewi. Ndoa yao inasambaratika kabisa (uk. 80).

Kamene anajaribu kuwasiliana na Lusweti kuhusu mamlaka aliyo nayo mamake Lusweti ambayo yatamzuia Lusweti kukua. Lusweti anazua vurugu badala ya kuuwasilisha msimamo wake kwa upole (uk. 96). Lusweti pia, hataki kuulizwa na Kamene na anamwacha katika upweke (uk. 97). Inaonekana kuwa mawasiliano yao si mazuri kwa sababu msimulizi anasema,"...Ugomvi wao ulifikia kilele (au labda mpomoko)…." (uk. 98). Usemi huu unaashiria kuwa hawakuwasiliana kwa amani. Luweti anapomtoa Kamene hospitalini baada ya kujifungua, wanawasiliana kwa maneno machache. Lusweti hataki kuongea. Tunaarifiwa kuwa Kamene anapendekeza wazungumzie matatizo ya ndoa yao lakini Lusweti hataki, anaahirisha kila mara (uk.102).

Mke wa Mumbo anatumia lugha isiyokuwa na heshima kwa mume wake baada ya fedha alizokuwa ameweka akiba kumalizika. Mumbo anasema:

> "…mke wangu ananiita mzembe. Mbona siwezi kupata kazi kama wanaume wengine, wana nini ambacho sina. Ni mwanamume gani ambaye siwezi kukidhi jamaa yangu? Kwani ni mwanamume suruali tu. Na hata hiyo suruali si heri nivue nijiendee uchi?" (uk. 158).

Mawasiliano baina ya Mumbo na mke wake yanaishia kuwa fujo baada ya watoto kufukuzwa kutoka shuleni.

Kaminda anapomfahamisha Sasi kuwa amepata kujua kwamba, msichana aliyeishi na babu yake ni mwanawe wala si mpwa wake, wanazozana. Anapomwuliza Sasi mara ya pili, ugomvi unazidi. Sasi anamtusi Kaminda sana na hata kusema mambo ambayo hayaeleweki (uk. 174). Kaminda anashindwa kusema lolote na kujinyamazia. Kila mmoja wao anaendelea na kuwaza na kuwazua. Mawasiliano baina yao yamezorota kabisa.

Mawasiliano baina ya Purupesa na Truvessa yanaokenana kuwa na udhaifu wakati Truvessa anaongea na Lulu kuhusu tatizo la mume wake. Ni dhahiri kuwa hajawasiliana na Purupesa kuhusu matatizo yaliyo katika uhusiano wao. Anavichoma nusu ya vitabu vya Purupesa na kuuchanachana mswada wake ili kuonyesha kuchukizwa kwake na jinsi Purupesa anavyompuuza (uk. 221). Baada ya Truvessa kutoka *Avacado Wasp*, wanagombana, kupandishiana sauti, kulaumiana na hata kubamiziana milango kiasi cha picha zilizokuwa ukutani kuanguka. Aghalabu, Truvessa hampi Purupesa nafasi ya kuongea. Haya ni mawasiliano mabaya yanayokuwa na athari hasi katika ndoa yao.

### 3.3. WATOTO

Watoto katika jamii zote zikiwemo za Kiafrika huendeleza kizazi. Njue, Rombo na Ngige (2007) wanaeleza kwamba, katika jamii za kiafrika ni lazima mtu aliyekomaa aoe na kupata watoto ili atambulike kwamba amekamilika. Wanaeleza kuwa watoto wa kiume wanapendelewa zaidi ya wale wa kike. Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* suala la watoto linaonekana kuwa changamoto katika ndoa kadhaa.

Miaka mitatu baada ya kufunga ndoa, Kitonga anaonyehsa kutoridhika kwake kwa Mwanamuka kutoshika mimba. Msimulizi anasema kuwa Kitonga anamlaumu Mwanamuka kwa maneno ya kila aina (uk. 69). Baada ya Mwanamuka kufanyiwa uchunguzi, daktari hapati tatizo lolote na anapendekeza afanyiwe uchunguzi wa kina zaidi na hata itabidi Kitonga achunguzwe. Jambo hili linamghadhabisha Kitonga. Kuanzia hapo, uhusiano wao unaanza kuzorota na Kitonga anaishia kumpachika mimba kijakazi wao. Baada ya vurugu na kukosa kupatana na Kitonga, Mwanamuka anaondoka.

Lulu na Pipo wanakabiliwa na changamoto kwa kuwa Pipo anamtaka Lulu amzalie mtoto lakini Lulu hataki; anapendekeza wapate mtoto baadaye (Uk. 209). Lulu anakataa kuzitilia hisia za Pipo maanani na hata kumwuuliza Pipo ikiwa kwa kweli shinikizo la kupata mtoto ni lake au ni la mamake Pipo. Uhusiano wao unaendelea kuzorota.

Kasina alitaka kuzingatia jadi ya babu na baba yake, kuoa zaidi ya mke mmoja na kupata watoto wengi (uk. 238-239). Kwa jumla, ana wake watatu. Imetajwa kuwa hapo awali alikuwa na nia na kumwacha mke wake wa pili, Maria kwa kuwa hakupata mtoto (uk. 247). Kama Maria hangejaliwa kupata mtoto, ndoa yake na Kasina ingevunjika.

Jinsia ya watoto nayo ni changamoto inayokabili baadhi ya ndoa. Kuna upendeleo wa watoto wa kiume kuliko wa kike. Kamende anapoambiwa na mkewe kuwa ni mja mzito, anaikubali "...hali hii kwa matumaini kuwa atapata mvulana mwingine wa kuongeza kikosi chake cha wanaume" (uk.89). Hata anaenda kusherehekea jambo hilo. Mke wake anapojifungua mtoto wa kike, anachukizwa na jambo hilo kiasi kwamba hampi mtoto

jina kama ilivyokuwa desturi. Mama yake anamwita Kamene, jina la majazi linaloonyesha jaala yake, kuwa anachukiwa (uk. 90). Anapokua, anaenda shuleni lakini baba yake hamkubalii kusoma zaidi ya masomo ya shule ya msingi ingawa ni mwerevu. Kwa kuwa Kamende amemkataza mtoto huyo, Kamene, amalize masomo yake, mhubiri wa kanisa analohudhuria mama Kamene anajaribu kumshawishi Kamende. Kamende anatishia kumkataza mama Kamene kwenda kanisani tena (uk. 90).

Swala la jinsia ya watoto linajitokeza katika ndoa za Kasina na wake wake ingawa halijazungumziwa kwa urefu. Wengi wa watoto anaopata nje ya ndoa ni wavulana ingawa hajawahi kupata mvulana na wake zake. Anaona hili kuwa ni kinaya (uk 252-253).

Katika ukurasa wa 232, kumetajwa kisa cha profesa wa saikolojia ambaye anamfukuza mkewe kwa kuwa hajifungui watoto wa kiume. Hii ni kuonyesha kuwa swala la watoto ni swala linalowaathiri na kuwagusa hata wasomi ambao wanatarajiwa kuyaelewa maswala ya uzazi.

## 3.4 KUKOSA UAMINIFU KATIKA NDOA

Uaminifu ni suala muhimu sana katika ndoa. Wakati wa kufunga ndoa ya kikristo, maharusi huhitajika kuapa kuwa watakuwa waaminifu kwa wenzao wa ndoa. Kutokuwa mwaminifu hutia doa katika ndoa yao. Chapman (2008:169-170) anasema kuwa sifa ya kupendelea uaminifu katika ndoa imejikita katika ubinadamu wetu, na inahusika na uadilifu na unyoofu. Kulingana na sheria za Kenya juu ya masuala ya ndoa (1962:7),

panapo ushahidi dhahiri kuwa mwanandoa si mwaminifu, mwenzake anaweza kumtaliki au adai kutalikiwa.

Ndoa ya Mwanamuka na Kitonga imeathiriwa na kutoaminika kwa Kitonga (uk 70). Kijakazi wao anashika mimba ya Kitonga. Mwanamuka anajaribu kuitetea ndoa yake lakini hafaulu. Anaamua kutoka kwa Kitonga.

Daphina anashiriki katika uzinzi na Kasu, rafiki ya mumewe. Kitendo hiki kinashuhudiwa na Mumbo, ambaye ni mtoto wa kaka ya mume wake Daphina (uk. 148-152). Baada ya muda fulani, Daphina anamwacha mumewe na kuivunja ndoa yao.

Pasta anashiriki katika uzinzi na mke wa mzee wa kanisa (uk. 152-153). Hii ni dalili kuwa ukosaji wa uaminifu ni changamoto inayowakabili watu wa matabaka yote wakiwemo wahubiri na wazee wa kanisa. Hiki ni kinaya kwa sababu wao ndio huwaapisha wanandoa kuwa waaminifu.

Truvessa anafanya kazi ya kuwatumbuiza wateja katika klabu ya *Avocado Wasp*. Anawatia wateja ashiki kwa mitindo yake ya kucheza densi. Kulingana na Amissah (2005:3-4) huu ni ukahaba na kwa hivyo Truvessa anakosa sifa ya uaminifu katika ndoa, jambo linalombughudhi sana Purupesa.

Klabu wanayoifungua Kasina na wenzake na ambako watu wanaenda kutumbuizwa na kusingwa misuli na wasichana wenye asili mbalimbali, inaendeleza ukosefu wa uaminifu

katika ndoa nyingi. Weitzer (2000:1-10) na Amissah (2005:3-4) wameeleza ukahaba kama vitendo vyote vinavyofanywa kwa nia ya kumtia mtu asiye mwenzi wa ndoa ashiriki katika ngono kwa maksudi ya kupata malipo. Weitzer (ibid) ameuainisha ukahaba katika vikundi viwili, ukahaba wa ndani na ukahaba wa nje. Katika kufafanua ukahaba wa ndani, anaueleza kama vitendo kama vile densi za nusu uchi na kuvua nguo, na usingaji misuli unaotia ashiki. Msimulizi anaeleza kuwa waliokuwa ukumbini wa *Avocado Wasp* ni wanaume na anaeleza athari za densi iliyokuwa ikichezwa na jinsi wateja walivyotoa pesa kuwapa wachezaji densi (uk 227).

Ndoa za Kasina na wake zake zinakabiliwa na changamoto ya kukosa uaminifu. Kulingana na msimulizi, Kasina ana uhusiano na wanawake wengine nje ya ndoa yake ili kutosheleza ashiki yake. Analala hata na vijakazi wa mke wake na kuwafanya wajawazito. Hata dawa za kienyeji anazojaribu kutumia mke wake ili kuirekebisha hali hiyo hazifai. Watoto wake ni wengi sana (uk. 238-241) na wanakwenda kwake nyumbani kutafuta haki zao (uk. 253). Mzee Usina anaandaa sherehe ili aitumie kumwonyesha Kasina kuwa hakuna mke ambaye hajawahi kushiriki katika uzinzi. Wanawake ambao hawakuwa na mahusiano nje ya ndoa zao ndio wangeula utumbo ulioandaliwa. Nyanya yake Kasina, mama yake na mke wake anayemwamini hawauli utumbo ule (Uk.243-244). Wake wa Kasina wanahisi kuwa mume wao amewaaibisha na wanapanga kulipiza kisasi (uk. 244).

Mwanasiasa mzee, aliyestaafu anaelezwa magazetini kama "….kielelezo cha kiongozi aliyeithamini familia sana na mmoja wa wanasiasa ambao hawakuwa na baa wala dosari

ya tabia...” (uk. 235) anamzuru Purupesa na kuungama kuwa ndiye baba yake mzazi. Ni dhahiri kuwa huyu mzee hakuwa mwaminifu kwa mke wake kama ilivyoripotiwa na vyombo vya habari.

**3.5 HILA NA UDANGANYIFU**

Baadhi ya wanandoa wanatumia hila na udanganyifu ili kutimiza haja zao. Hii ni changamoto kwa asasi ya ndoa kwa kuwa athari zake ni hasi na aghalabu ni chanzo cha changamoto zaidi.

Agusto anatumia hila na udanganyifu ili kupata fedha za kutumia kunywea pombe na kucheza kamari. Anajaribu njia zote ili apate pesa. Unywaji pombe unampelekea kupata ugonjwa wa ini unaosababisha kifo chake.

Baada ya Lusweti kumpiga Kamene kwa kutomwandalia chakula haraka anajifanya kuwa anasikitika na kuomba msamaha. Kamene anamwamini na kumsamehe lakini msimulizi anaeleza kuwa Lusweti habadiliki. Anaendelea kumdhulumu na kumkandamiza mkewe, Kamene (uk. 102-106).

Sasi anatumia hila na udanganyifu ili aolewe na Kaminda. Anaenda kwa Kaminda na kumwambia kuwa anatafuta usaidizi kwa kuwa amefukuzwa pale alipokuwa anaishi (uk. 164). Kaminda anagundua kuwa Sasi hana nia ya kuhama (uk. 165), na ameshakuwa mke wake. Baadaye, Kaminda anagundua kuwa Sasi ana mtoto ambaye amekuwa akidai kuwa ni mpwa wake (uk. 170-171). Sasi anatumia hila ili agundue kinachomsumbua

Kaminda (uk 172-173). Baada ya uchunguzi zaidi, Kaminda anagundua kuwa Sasi ana nia ya kulipiza kisasi ndipo anamfanyia hila hizo.

Betty anaenda kwa Wamae na kusema kuwa anatafuta kazi. Hatimaye, Wamae anamwoa. Baada ya biashara za Wamae kuporomoka ndipo anagutuka kuwa Betty ndiye aliyekuwa katibu muhtasi wa zamani wa mbunge wao (uk. 192). Inaonekana kuwa Betty ametumwa na mbunge huyo ili azijue siri zote za Wamae ili kumporomosha.

### 3.6 MILA NA DESTURI ZILIZOPITWA NA WAKATI

Utamaduni hubadilika jinsi nyakati zinavyoathiriwa na mabadiliko ya kiteknolojia na utandawazi. Jamii ya riwaya hii ni ya mwishoni mwa karne ya ishirini. Inakumbwa na changamoto ya kuzingatia mila na desturi zao za jadi pamoja na kuwepo haja ya kufumbata usasa. Changamoto hii ina athari hasi katika baadhi ya ndoa zilizoko katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*

Kutokana na ushauri wa babake Kasekesi kwa bintiye, tunang'amua kuwa ana mtazamo wa kiubabedume unaowapendelea na kuwatukuza wanaume na kuwadunisha wanawake. Anauthamini utamaduni wa jamii yake na anakataa kuufumbata usasa. Anathamini tohara ya wanawake, mamlaka ya mwanamume juu ya mwanamke, adhabu kwa mwanamke na unyonge wa mwanamke (uk. 47-48). Mtazamo huu pia unajidhihirisha kwa Lusweti anayejichukua kama mwinyi wa kuhudumiwa na mke. Pia, anamchapa mke wake kwa kutozingatia mila na desturi za jamii yao (uk, 102- 103).

Athari ya kushikilia imani zilizopitwa na wakati zinajitokeza katika ushauri wa mama ya Kasekesi kwa binti yake. Ni dhahiri kuwa haifurahii ndoa yake (uk. 43-46).Utamaduni unamnyima mke nafasi ya kutoa maoni yake katika ndoa. Kasekesi hasemi lolote Agusto anapolalamika kwa sababu Getonga anaomba msaada. Kasekesi anasema kuwa mke hawezi kusema lolote kwa sababu yeye "… ni mtu wa kuja." (uk. 53).

Mila na desturi za Kiafrika katika riwaya hii zinathamini watoto na ikiwa mtu hajapata mtoto, huchukuliwa kuwa hajakamilika (Njue et al; 2007). Kwa baadhi ya watu katika jamii, thamani ya mwanamke ni katika idadi ya watoto ambao atawazaa. Mwanamuka anadharauliwa na mumewe na aila yake kwa kuwa hajafanikiwa kupata mtoto. Ndoa yake inavunjika kwa sababu hii.

## 3.7 UTANDAWAZI

Utandawazi ni mshikamano wa kimataifa unaotokana na kubadilishana bidhaa, teknolojia na nyanja nyingine za utamaduni. Hali hii imerahisishwa na usafiri wa haraka na mawasiliano, ambazo zimerahisisha mtagusano baina ya watu wanaoishi maeneo tofauti ya kijiografia. Athari za utandawazi zinaonekana katika asasi ya ndoa. Baadhi ya ndoa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* zimekumbwa na changamoto ya utandawazi na njia ambazo wanandoa wahusika wanakabiliana nayo, zinasababisha kusambaratika kwa ndoa.

Mumbo anaipoteza kazi yake katika kiwanda cha mafuta baada ya mfumo wa kiuchumi wa soko huria kuanza. Viwanda vingi vinafungwa, kwa hivyo, ni vigumu kupata kazi

nyingine. Mkewe anakosa kuielewa hali ya kiuchumi ya nchi yao na pia kumwelewa mumewe mwenyewe. Anadhani kuwa Mumbo ni mzembe na mdanganyifu. Anatoroka na watoto wao wote (uk. 158-160).

Wamae, aliyekuwa maskini, anaanzisha biashara ndogo ili kujikimu. Anapanua biashara yake kulingana na mitindo ya ulaji ya wateja wake. Mfumo wa soko huria unapoanza, anaanza kuagiza bidhaa kutoka nchi za nje na kuwaajiri vijana wengi wanaozungusha bidhaa maofisini. Anajikita zaidi katika biashara yake na kuadimika nyumbani kwake. Kuadimika huku kunaathiri ndoa yao kwa njia hasi (uk. 187).

Athari ya utandawazi kiutamaduni inaonekana kupitia mhusika Truvessa anayetaka Purupesa amwonyeshe mapenzi kwa njia za kisasa kama kumletea maua ya *Valentine*, akumbuke siku yake ya kuzaliwa, amnunulie kadi yenye mishale ya *cupid* na kadhalika, Truvessa anahisi kuwa Purupesa hamthamini (uk. 230). Truvessa pia, anawatumbuiza wateja katika klabu ya kisasa kwa kucheza densi na kuwatia wateja ashiki wakiiga mitindo ya nchi za ng'ambo. Klabu hii ni ya mheshimiwa Kasina. Anapoulizwa na Purupesa, lugha anayotumia inaonyesha athari za ufeministi wa kiharakati ulioanzia Marekani (Uk. 232-233). Uhusiano katika ndoa yao unazorota vibaya.

Athari za utandawazi katika utamaduni inaonekana kupitia mhusika Lulu ambaye amejiunga na kikundi cha wanawake ambao wanazingatia ufeministi wa kiharakati. Kwa kuwa anahisi kuwa Pipo anaubana uhuru wake, Lulu anataka waachane. Hatimaye, wanaachana (uk. 206-210).

Kulingana na msimulizi wa hadithi, utamaduni wa kutumia na kutupa unajitokeza katika ndoa. Anasema:

> "Ni kama mahusiano ya watu kwenye ndoa yamekuwa sawa na mahusiano ya waajiri na waajiriwa-yanakatika haraka haraka tu. Ni kama maisha ya binadamu yameingia kwenye awamu ya 'mahusiano ya muda mfupi'. Labda ule utamaduni wa 'kutumia na kutupa kama yale masahani ya plastiki au vikombe kwenye harusi umevuka ngazi nyingine. Kila kitu kimekuwa cha muda mfupi…Ndoa za muda mfupi…
> ( uk. 103-104).

### 3.8 MAGONJWA

Baadhi ya ndoa zilizomo katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* zinakabiliwa na changamoto ya magonjwa yanayoathiri viungo muhimu katika mahusiano ya mke na mume na matatizo mengine ambayo hayashughulikiwi kwa njia zifaazo na kwa hivyo, kuifanya hali ya mhasiriwa kuwa mbaya zaidi na kwa hivyo, kuwa changamoto katika ndoa yake.

Nyakor anapata uvimbe katika ziwa lake. Kwa kuwa daktari wake amesafiri, mume wake anazitumia fedha alizokuwa ameweka akiba kwa matibabu ya Nyakor. Jambo hili linapelekea Nyakor kwenda hospitali ya umma anakofanyiwa uchunguzi duni na daktari kupendekeza ziwa likatwe kwa kuwa uvimbe ni wa maradhi ya saratani. Nyakor anakatwa ziwa ambalo linafanyiwa utafiti baadaye, na inapatikana kuwa uvimbe haukuwa saratani bali kinyungi cha kawaida.Tukio hili lina athari hasi za kisaikolojia kwa Nyakor. Badala ya mume wake kumfariji, anaanza kuadimika nyumbani.Hatimaye uhusiano wao unazorota kabisa. Kabla ya Nyakor kukatwa ziwa, uhusiano wao ulikuwa mzuri, kwa hivyo matibabu duni ni sababu ya kusambaratika kwa ndoa yao.

Purupesa anakumbwa na tishio la kupata saratani baada ya kuwa na uvimbe wa korodani. Anatolewa korodani katika hospitali. Kutolewa korodani kunamwathiri kisaikolojia kwa kuwa amesikia kuwa upasuaji aliofanyiwa ni sawa na kuhasiwa.Kwa sababu hii mahusiano na mkewe yameathirika vibaya.

Anapata tatizo jingine la kisiha na daktari wake anapendekeza afanyiwe upasuaji. Kwa kuwa bima ya hospitali ya chuo ina matatizo, Purupesa anafanyiwa upasuaji katika hospitali ambayo haikuwa nzuri sana. Upasuaji huo unafanywa vibaya na kuharibu mshipa muhimu. Kwa maoni yetu athari za upasuaji huu zinamfanya Purupesa asiweze kutekeleza mambo fulani ya kindoa. Tunakisia hivyo kutokana na ujumbe Truvessa anaouacha anapomwacha Purupesa (uk. 234) Kama Purupesa hakuugua magonjwa yanayoathiri viungo vinavyohusika katika mahusiano ya unyumba, ndoa yake haingesambaratika.

Maria anapata tatizo la *obstetric fistula* kwa sababu ya kuolewa akiwa na umri mdogo na kupata maumivu ya kujifungua kwa muda mrefu. Mume wake anaogopa kuambukizwa maradhi hayo, akidhani Maria ameyapata kwa kuwa na mahusiano nje ya ndoa. Kwa hivyo, anamtelekeza. (uk 247-249). Kwa kutoshughulikiwa mapema wakati wa kujifungua, ndoa ya Maria na Kasina inazorota.

### 3.9 MAHUSIANO YA KIJAMII

Mfumo wa ujamaa katika jamii ya kimapokeo ya Kiafrika unasababisha uhusika wa kila mwanajamii katika maisha ya jamaa yake. Kila mmoja ana haki ya kusaidiwa kwa hali na mali na jamaa yake anaye uwezo; vilevile ni jukumu la mwenye uwezo kuwasaidia waliopungukiwa. Kwa kuwa katika desturi za kiafrika, mwanamke anaolewa na mwanamume, anachukuliwa kuwa hana mali yoyote na vitu vyote ni vya mumewe. Kwa sababu hizi, jamaa wanakuwa changamoto hasi kwa asasi ya ndoa. Changamoto hii inajitokeza katika baadhi ya ndoa zilizoko katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*

Ndoa ya Kasekesi inakumbwa na changamoto kutoka kwa jamaa zao. Agusto anaposafiri, anamwacha Kasekesi na jamaa zake, pengine wamchunge au kumdhibiti. Kulingana na usemi wa Kasekesi, waitumie mali ya ndugu yao (uk. 50). Katika ukurasa wa 52 hadi 53 Getonga anawatembelea Agusto na Kasekesi kwa madhumuni ya kupata pesa za kufanyia biashara. Anapozikosa, anakasirika sana. Anachukulia kuwa ilikuwa haki yake kupewa pesa hizo. Kulingana na matamshi ya Agusto, jamaa zake wana mazoea ya kuomba pesa kutoka kwake. Jambo hili linathibitishwa baada ya kifo cha Agusto wanapomlaumu

Kasekesi kwa Agusto kufilisika na kifo chake kwa kusema "…Alikuwa kama shamba letu la mzabibu!" (uk.57)

Jamaa za Kitonga wanaenda nyumbani kwa Kitonga na kumpiga vijembe Mwanamuka kwa kuwa hajafanikiwa kushika mimba. Kenzi, dada yake Kitonga, anamdhihaki wifi yake (uk 69). Yeye ndiye anayetumwa na Kitonga kumpasha Mwanamuka habari kuwa kijakazi wao ameshika mimba ya Kitonga. Zaidi ya kumpasha habari hii, anamtusi sana (uk. 69-70). Hii ni kuonyesha kuwa Kenzi na Kitonga wanashirikiana kumdhulumu Mwanamuka.

Uhusiano baina ya Lusweti na mama yake unaathiri ndoa ya Lusweti na Kamene kwa njia hasi. Mama ya Lusweti anamfulia nguo zote, pamoja na za ndani ( Uk 95-96). Lolote analouliza mama ya Lusweti kufanyiwa, anafanyiwa mara moja na Lusweti bila kujali hali ya kifedha ya familia yake. Kamene anahisi amenyimwa mamlaka kama mkewe Lusweti na nafasi hii imechukuliwa na mama mkwe (uk. 96). Fikra hii inadhihirika wakati Kamene anamwagiza Lusweti amwambie rafiki yake amtafutie kijakazi wa kumsaidia atakapojifungua. Mama ya Lusweti anasema kuwa atamtafuta kijakazi lakini hafanyi hivyo. (uk.98).

Ndoa ya Kaminda na Sasi inaathiriwa vibaya na changamoto ya jamaa za Sasi. Katika ukurasa wa 168, tunaambiwa kuwa Sasi anapodhani kuwa mume wake amemnyamazia, anawaalika jamaa zake kwenda kuishi nao. Hata hivyo, hapendelei jamaa wa Kaminda kwenda kwao kwa sababu alifikiri wanafika pale kumchunguza. Uhusika wa nyanya ya

Sasi katika kushirikiana na Sasi kuficha ukweli kuwa Sasi ana mtoto nje ya ndoa unaathiri pakubwa ndoa ya Sasi na Kaminda. Huu ndio mwanzo hasa, wa kusambaratika kwa ndoa yao kwa sababu Kaminda anapofahamishwa jambo hili, anaanza kufanya uchunguzi na anagundua mengi (uk. 174).

Wakati wa Pipo na Lulu kuhalalisha ndoa yao kwa kulipa mahari, jamaa za Lulu wanaitisha mahari mengi kwa kuwa Lulu alikuwa amesoma hadi viwango vya juu. Jamaa zake wanadai walimsomesha kwa taabu na dhiki (uk. 204), ingawa uhalisi ni kuwa Pipo amehusika sana katika masomo ya Lulu (Uk. 200-201). Baadaye, Pipo anapomwuliza Lulu sababu yake ya kutosema lolote, anasema kuwa mama yake alitishia kumlaani ikiwa atapinga uamuzi wa jamaa zao. Pipo anapopendekeza waende kufunga ndoa kwa mkuu wa wilaya, Lulu anasema kuwa baba yake na nyanya yake wataathiriwa vibaya. Pipo anafanya juhudi kutafuta mahari yanayohitajika. Baada ya kumwoa Lulu, anafanya kazi kwa bidii na kuanzisha biashara nyingi ili kufidia pesa alizotumia kulipia mahari (uk. 208). Anatumia wakati mwingi katika biashara hizo na hivyo uhusiano baina yake na Lulu unazorota vibaya. Kwa maoni yetu, kama jamaa za Lulu hawangedai fedha nyingi za mahari, Pipo hangezitafuta mbinu za kufidia fedha hizo, na hivyo, uhusiano wao haungesambaratika hatimaye.

## 3.10 UKOSEFU WA HISIA

Baadhi ya ndoa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* zinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa hisia hasa katika mahusiano ya mume na mke pengine kwa kuzoeana na hali kadhalika, kusinywa kwa mwanandoa mmoja, au wote wawili.

Nyakor anapojaribu kuwasiliana na mume wake juu ya suala hili nyeti, mume wake hakubaliani naye. Msimulizi wa hadithi anasema:

> “Mume akabisha kwa kusema ndoa haina nafasi ya uhisivu wa ujana; wayaendeleze mapenzi yao tu - ni kama moto wa kifuu tu, unaobaki ndani kwa ndani.” (uk.79)

Nyakor hakubaliani naye na analinganisha mahusiano ya aina hii utaratibu wa kimtambo lakini anatumia lugha ya kiingereza. Ndoa yao inasambaratika kabisa.

Baada ya Kamene na Lusweti kufunga ndoa, wanaendelea vyema kwa muda fulani kisha ndoa yao inaanza kusambaratika. Hisia katika mahusiano yao kama mume na mke zinaathirika.

> Hata kujiacha huria wanapohusiana kimwili kukawaadimu na mahusiano yao, kama mume na mke, badala yake mapenzi yao yakabakia kama kiviga fulani ambacho wanakifanya kimya kimya kama watambikaji wanaotoa kafara bila ya kujua kama mzimu wataikubali au la. Kimya kimya kama mhubiri anayeongoza ibada ya wafu.

> “Mambo hayo yalikuwa ya zama zile…kwenye Ndoa mambo yanaenda kwa ada…ni kama ibada za Jeshi la wokovu…kila kitu mahali pake!” akasema mchekeshaji. (uk.96-97)

Ndoa nyingine zinazokabiliwa na ukosefu wa hisia ni ile ya Kassim na Betty (uk. 187-188) na ile ya Kasina na mke wake mmoja (uk.239).

**3.11 HITIMISHO**

Katika sura hii, tumezichanganua changamoto zinazoikabili asai ya ndoa ziliomo katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* Tumeona kuwa ndoa zote zinakabiliwa na changamoto nyingi. Hizi ni dhuluma na ukatili, ukosefu wa mawasiliano bora, jinsia ya watoto na kutozaa watoto, uzinzi, hila na udanganyifu, utamaduni uliopitwa na wakati, utandawazi, magonjwa, uhusiano wa jamii na ukosefu wa kuhisi. Baadhi ya njia wanazotumia wahusika wa ndoa kukabiliana na changamoto hizi zinazifanya ndoa zao kusambaratika na wakati mwingine, kuvunjika. Kwa hivyo, asasi ya ndoa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* imesawiriwa kuwa inakumbwa na changamoto nyingi zinazoifanya kusambaratika. Utafiti wetu unalingana na wa Mbuthia (2005:119-125) aliyetafitia hadithi fupi za Kiswahili na kupata kwamba asasi ya ndoa imekumbwa na changamoto nyingi kama vile uzinzi mwingi, kutotosheka katika maisha, matumizi ya dawa za kienyeji ili kumnata mwenzi wa ndoa, kutowajibika, hila, dhuluma na kutelekezwa.

# SURA YA NNE

# MIKAKATI YA KUIOKOA ASASI YA NDOA

## 4.0 UTANGULIZI

Katika sura ya tatu tumezichanganua changamoto zinazoikabili asasi ya ndoa na kuisambaratisha katika riwaya ua *Unaitwa Nani?* Kwa vile fasihi ni zao la mazingira ya mwandishi wa kazi inayohusika, ni dhahiri kuwa changamoto hizi za ndoa zinaikabili jamii ya karne ya ishirini na moja.

Ingawa asasi ya ndoa inakabiliwa na changamoto zinazotishia kuisambaratisha kabisa, baadhi ya mikakati inayotumiwa au kutajwa na wahusika inaweza kuchangia kwa jinsi chanya kuiokoa asasi hii.

Katika sura hii, tumechanganua mikakati chanya ya kuiokoa asasi ya ndoa iliyo katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*. Pia, tumelinganisha mikakati hii na maoni ya wataalamu mbalimbali kama vile wanasosholojia, washauri nasaha na wataalamu wa musuala ya ndoa.

## 4.1 UWAZI NA MAWASILIANO

Ndoa nyingi katika riwaya ya *Unaitwa Nani*? zinakabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa mawasiliano mazuri. Wahusika kama vile Kamene, Mumbo na Purupesa wanajaribu kuziokoa ndoa zao kwa kuweka mikakati ya mawasiliano mema.

Kulingana na Burleson na Denten (1997:884), mawasiliano ni wajibu muhimu katika ndoa. Kwa sababu hii, kila mwanandoa anahitajika kuwasiliana kwa njia chanya na mwenzake wa ndoa. Chapman (2008:116) anaeleza ikiwa mwanandoa ana mfumo hasi wa mawasiliano, mwenzake ana jukumu la kuubadilisha mfumo huu hasi na kuubadilisha uwe chanya, hasa kwa kumsikiza mwenzake vyema. Mawasiliano mema huwawezesha wanandoa kuelewana vyema na kuondoa mawazo na hisia hasi (Amulega na Amulega: 2009; 61-62).

## 4.2 USHAURI NASAHA

Tumeona kuwa ili ndoa ifanikiwe lazima pawe na mawasiliano bora ili pawe na uelewano. Kuna matatizo yanayozuia mawasiliano bora na hali kadhalika kudhoofisha nyanja nyingine za ndoa. Mifano ni magonjwa yanayoathiri sehemu zinazohusika na mahusiano ya ndoa, kama yale yaliyowakumba Nyakor (uk 78-79), Purupesa (uk.220) na Maria (uk.249). Mfano mwingine ni matukio mabaya yaliyomfanyikia mtu na kumwathiri kisaikolojia kama vile Purupesa (Uk. 220-221).

Baadhi ya wahusika wameonyesha umuhimu wa wataalamu kama vile madaktari na washauri nasaha, kuchanganua hali zinazowakabili wahusika na kuwashauri; na hali kadhalika kuzinusuru ndoa zao. Mifano ni Nyakor anaposisitiza umuhimu wa wao kumuona mtaalamu wa ushauri nasaha (uk.78-79), Betty alipomwendea Dr. Thetis kupata ushauri juu ya ndoa yake, Maria alipoenda kupata ushauri kwa Bw. Mpiro na Truvessa anaposema, "… si mwanasaikolojia wa kuchanganua nafsi za wanaume…." (uk. 221)

Chapman (2008:12) anaashiria kuwa ushauri nasaha una manufaa kwa ndoa anaposema kuwa yeye huridhika anapowaona wanandoa aliowashauri wakipiga hatua changa katika ndoa zao.

## 4.3 MATIBABU YANAYOFAA

Wahusika wawili katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*, Nyakor na Purupesa wanapata matibabu duni yanayopelekea kuzorota kwa ndoa zao. Kama wangepata matibabu yaliyofaa ndoa zao hazingesambaratika. Mwanamuka anaenda kwa daktari kufanyiwa uchunguzi, ikiwa ana kasoro inayomzuia kuzaa. Daktari hapati kasoro na kupendekeza mume wake afanyiwe uchunguzi pia.

## 4.4 HISIA KATIKA NDOA

Hisia chanya ni muhimu katika ndoa. Baadhi ya wahusika katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* wanatambua jambo hili. Mama ya Kasekesi anamshauri Kasekesi:

> "Mtafute mwanamume … anayekuthamini
> kama kiumbe mwenye hisia na hisia kama
> hujui ni chanzo cha uhai wenyewe." (uk.43)

Nyakor, wakijadiliana na mume wake juu ya mahusiano, yao anasema:

> "...mapenzi, ni mwana mkembe huhitaji
> kuengaengwa na hata kuimbiwa bembelezi;
> hajasikia chombezi wanazoimbiwa wapenzi
> na wenzi wao? Si swichi au jiko la gesi
> ambalo unazima kasha kuwasha napotaka….

> Hajamwona hata Jogoo, na kuku ambaye tofauti na binadamu hana akili, anachezeshacheze bawa lake kumbembeleza koo au kumbikumbi anafuatana unyounyo na mwenzake, wakapanda na kushuka, kupenya huku na kule?...” (Uk.79)

Baba ya Kaminda akimshauri Kaminda juu ya ndoa alimwambia:

> “…ndoa ni biashara ya hisia kati ya mwanamume na mwanamke.” (uk.163)

Maana ya kauli hii ni kwamba inapasa kila mwanandoa kudhihirisha hisi chanya kwa mwenzake. Amulega na Amulega (2009:116) wanasema kuwa mume na mke wanatakiwa kujiacha huria katika mahusiano yao ya ndoa. Burke (2007:7) anawashauri wanandoa kutiana ashiki ili kukamilisha mahusiano yao ya ndoa,

## 4.5 MSAMAHA

Ndoa nyingi za wahusika wa riwaya ya *Unaitwa Nani?* zinaanza kwa furaha kuu. Amulega na Amulega (2009:31) wanasema kuwa hii ni hatua ya kwanza ya ndoa ambayo ina raha na furaha nyingi. Hatua ya pili ya ndoa ni matatizo na mwanandoa anaanza kuziona ila za mwenzake. Katika hatua hii wanandoa hukosana mara kwa mara kwa kuwa hawajaelewana vyema. Pia, binadamu wanapokuwa katika jamii, kukosana ni jambo la kawaida. Aliyekosewa huwa na uchungu. Hata hivyo, msamaha huundoa uchungu kutoka kwa aliyekosewa, na aliyekosa huacha kujilaumu.

Baadhi ya wahusika katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* wanajizatiti kutumia msamaha kuzinusuru ndoa zao. Hawa ni Lusweti na Kamene (uk.103), Kaminda (uk.174), Purupesa (uk 221, 233 na 236). Kwa mujibu wa Chapman (2008:179), msamaha ni muhimu katika kuiponya ndoa baada ya mtafaruku kuwepo.Anaendelea kusema kuwa msamaha una sifa mbili muhimu. Hizi ni; aliyekosa kuomba msamaha, na aliyekosewa kumsamehe mkosaji kutoka moyoni mwake.

Wanandoa wakifanya hivyo, watazistawisha ndoa zao. Amulega na Amulega (2009:169) wanaafikiana na Chapman(ibid) na kuongeza kuwa msamaha husababisha upendo baina ya wanandoa kuongezeka na hushawishi wanandoa kubadilisha mienendo mibaya.

## 4.7 UVUMILIVU, UELEWANO NA USHIRIKIANO

Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* kuna ndoa moja ambayo imestawi. Hii ni ndoa ya Makula na Nzesi ambao ingawa ni mafukara, ndoa yao ni imara.Kamene anakumbuka jinsi Makula na Nzesi wanavyosumbuka kupata riziki lakini ndoa yao imedumu.

> “Uwezo wao wa kiuchumi ni wa chini sana lakini hakuna asiyejua jinsi anavyopendana watu hawa. Na mpaka leo ndoa yao ingali inadumu;wao ni ule mkono unaosemwa mtupu lakini unaorambwa….”(uk. 103-104)

Msimulizi ameisawiri ndoa hii kama kielelezo chema katika jamii. Ndoa hii inampa Kamene matumaini kuwa ndoa yake na Lusweti yaweza kufanikiwa; anatia juhudi lakini Lusweti hawajibiki na kwa hivyo ndoa yao inasambaratika.Ndoa nyingine ambayo imedumu ni ile ya Mswahili, inayotajwa na Pipo. Ndoa hizi mbili zinalingana na ndoa ya wahusika Myombekere na Bugonoka katika riwaya ya Aniceti Kitereza ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Ntlanawe na Bulihwali (juzuu la kwanza)* iliyotafitiwa na Mbatiah (1999:190-193).

Amulega na Amulega (2009:169, 89,125) wanaeleza umuhimu wa uvumilivu, uelewano ushirikiano na kujitolea katika kuistawisha ndoa.

## 4.7 THAMANI YA NDOA

Baadhi ya wahusika katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* wameifanya asasi ya ndoa kuwa kitegauchuni ili kujifaidi kifedha. Hawa ni wazazi wa Mwamuka (uk.68), babake Kasekesi (uk.48), mke wa Mumbo (uk.158) na jamaa za Lulu (uk.202-208). Kwa kufanya hivi wanaikosa thamani halisi ya ndoa.

Mugambi na Kirima (1976:46-47) wanasema mahari ni mali anayopewa baba ya msichana na mwanamume na jamii yake kabla ya kumuoa msichana huyo, wala si bei ya kumnunua. Mahari yana uamilifu wa anayeoa kuonyesha hadharani kuwa amemfurahia msichana huyo kama mke. Mahari hutia chapa ndoa hiyo hadharani. Amulega na Amulega (2009:16) wanasema kuwa siku hizi wazazi wanaweza kuitisha mahari nyingi sana, hasa ikiwa msichana amesoma hadi ngazi za juu au ana kazi iliyo na mshahara mzuri. Kulingana na Haselbarth (1976:81-82) kwa kuitisha mahari nyingi, hadhi na

thamani ya msichana hupunguka kwani ni kama msichana amenunuliwa. Anaongeza kuwa kilichonunuliwa hatimaye, chaweza kutupwa baada ya kutimiza uamilifu wake.

## 4.8 KUACHA MILA NA ZILIZOPITWA NA WAKATI

Jamii ya karne ya ishirini na ishirini na moja inakumbwa na mabadiliko ya kasi. Jinsi nyanja kama vile uchumi, elimu na siasa zinavyobadilika, ndivyo utamaduni na thamani za jamii zinavyobadilika.Baadhi ya desturi zinazozingatiwa na wahusika zimepitwa na wakati. Desturi hizi ni kama vile tohara ya wasichana, ndoa ya lazima, ubabedume, kuchapa mabibi na kupendelea watoto wa kiume zaidi ya wa kike.

Mamake Kasekesi anaonekana kuelewa kuwa utamaduni unabadilika anapomshauri Kasekesi. Anasema:

> "…utamaduni si jabali linalokwama pale pale, hubadilika kama mmea unaokua…."
> (uk.43)

## 4.9 UAMINIFU

Katika jamii za Kiafrika uaminifu katika ndoa hasa kwa wanawake ni thamani. Katika sherehe za ndoa za kisasa hasa za kikristo, wanaofunga ndoa huapa kuwa waaminifu kwa wenzao wa ndoa. Mwanandoa anapokuwa na mahusiano nje ya ndoa, anavunja ahadi aliyotoa.

Chapman (2008:170) anaeleza kuwa kuna uwezekano kuwa hakuna jambo jingine linalomtia uchungu mtu binafsi na linalodhuru ndoa kama kugundua kuwa mwenzake wa ndoa amekuwa na mahusiano nje ya ndoa. Anaongeza kuwa ukosefu wa uaminifu hutikisa kiini cha umoja katika ndoa.

Kwa maoni yetu, ingawa jamii ya leo inakumbwa na mabadiliko ya kasi ya kuitamaduni, ni vyema kuchanganua yale ambayo ni hasi kwa asasi ya ndoa na kutoyakumbatia. Mifano ni vuguvugu la kupigania haki za wanawake na hali kadhalika kusambaza ufeministi wa kiharakati, na kuwachezea wateja dansi ili kupata pesa. Pia, yapasa kila mwanandoa kuiweka ahadi anayoitoa wakati wa kufunga ndoa.

## 4.10 UHUSIANO WA KIJAMII

Tumeona jinsi jamii inavyochangia kusambaratisha asasi ya ndoa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*. Hata hivyo, kuna wanajamii wachache katika riwaya hii wanaotia juhudi chanya ili kuiokoa asasi ya ndoa. Juhudi hii inajidhihirisha kwa ushauri wanaowapa wanandoa. Mifano ni babake Mumbo anapomshauri Mumbo juu ya ndoa (Uk. 154-155), Pasta anapomshauri Kaminda juu ya ndoa (uk.165,172,174) na wazazi wa Kasina wanapomshauri juu ya tabia zake za ukware na kumtelekeza mke wake, Maria (uk.241, 244,249).

Amulega na Amulega (2009:42-44) wanashauri wanandoa kuishi peke yao mwanzoni mwa ndoa yao ili wapate kujuana vyema. Wanaendelea kusema kuwa ni jukumu la mwanandoa kumpa mwenzake katika ndoa  nafasi ya kwanza, juu ya watu wengine ili

kudumisha umoja katika ndoa yao. Wakifanya hivyo, ndoa yao itastahamili magumu yatakayoipata.

## 4.11 HITIMISHO

Katika sura hii, tumeichanganua mikakati ambayo baadhi ya wahusika katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* wanatumia au kutaja kwa madhumuni ya kuikoa asasi ya ndoa. Hii ni uwazi na mawasiliano, kutafuta ushauri nasaha, matibabu yanayofaa, nafasi ya hisia katika ndoa, kuomba na kutoa msamaha, kutia maanani thamani ya ndoa, kuacha mila zilizopitwa na wakati, uhusiano mwema katika jamii, uaminifu katika ndoa na uvumilivu, uelewano na ushirikiano.

Katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* asasi ya ndoa imesawiriwa kama asasi inayokumbwa na changamoto nyingi zinazoisambaratisha. Hata hivyo, mwandishi ameonyesha kuwa bado kuna matumaini ya kuiokoa asasi ya ndoa. Amedhihirisha kauli ya Albrecht (1954:425) kuwa fasihi huathiri jamii; asasi ya ndoa katika jamii ya karne ya ishirini na moja imekumbwa na changamoto nyingi lakini kuna matumaini ya kuiokoa. Tumelinganisha matokeo ya uchunguzi wetu na kauli za wataalamu mbalimbali na kuthibitisha kuwa mikakati hii yaweza kuiokoa asasi ya ndoa. Hali kadhalika, tumethibitisha kuwa riwaya ya *Unaitwa Nani?* imeweza kuisawiri asasi ya ndoa kama ilivyo katika jamii ya leo.

# SURA YA TANO

# TATHMINI NA MAPENDEKEZO

## 5.0 UTANGULIZI

Sura hii ndiyo hitimisho la utafiti wetu. Tumeyatathmini madhumuni yetu ya utafiti huu, ikiwa tumefaulu kuyatosheleza au la. Pia, tumezitathmini nadharia tete zetu. Hatimaye, tumetoa mapendekezo ya utafiti zaidi kuhusu riwaya ya *Unaitwa Nani?*

## 5.1 MADHUMUNI YA UTAFITI

Katika utafiti wetu, tumehakiki maudhui ya usawiri wa asasi ya ndoa katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* tukitumia nadharia ya sosholojia ya fasihi. Sababu ya kuchunguza usawiri wa asasi ya ndoa katika riwaya hii ni kuwa mwandishi wa riwaya hii ameangazia mivutano baina ya wanaume na wanawake katika jamii ya riwaya, ambayo inawakilisha jamii ya leo. Kwa kuwa ndoa ni asasi ya jamii, imechukua nafasi kubwa sana na kuangaziwa kwa kina. Riwaya hii ina sehemu mbili. Sehemu ya kwanza imeangazia jinsi wanaume wanachangia kusambaratisha asasi ya ndoa; nayo sehemu ya pili imeangazia mchango wa wanawake kuisambaratisha asasi hii.

Tuna na madhumuni manne ya utafiti wetu. Madhumuni ya kwanza ni kutathmini mchango wa kila mwanandoa katika kuboresha au kusambaratisha ndoa yake. Katika sura ya pili, tumezichanganua ndoa zilizo katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* na tumechunguza mchango wa kila mwanandoa katika kuistawisha au kuisambaratisha ndoa yake. Tumegundua kuwa watu wa jinsia zote mbili wana uwezo wa ama kuziimarisha ndoa zao au kuzisambaratisha.

Madhumuni yetu ya pili ni kubainisha changamoto zinazoikabili asasi ya ndoa katika jamii. Asasi ya ndoa inasawiriwa kama asasi inayokumbwa na changamoto nyingi. Katika sura ya tatu tumezichanganua changamoto zinazoikabili na kuisambaratisha asasi hii katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* tukizingatia nadharia ya sosholojia ya fasihi, tumegundua kuwa changamoto hizi ndizo zinazoikabili asasi ya ndoa katika jamii ya leo. Changamoto hizi ni: dhuluma na ukatili, ukosefu wa mawasiliano bora, mwanamke kukosa kuzaa, jinsia ya watoto, kukosa uaminifu katika ndoa, matumizi ya hila na udanganyifu, kuzingatia mila desturi zilizopitwa na wakati, utandawazi, magonjwa, kusinywa na uhusiano mbaya wa jamii. Kwa hivyo, tumefaulu kuthibitisha madhumuni ya pili.

Madhumuni yetu ya tatu ni kuchunguza dhuluma dhidi ya mwamume na mwanamke katika asasi ya ndoa. Katika uchunguzi wetu (sura ya pili na ya tatu) tumegundua kuwa baadhi ya wahusika wanawadhulumu wenzao wa ndoa kimwili, kimapenzi au kisaikolojia. Wahusika hawa ni wanaume na wanawake kinyume na inavyoaminiwa na wafeministi kuwa wanaume ndio wanaowadhulumu wanawake na kusambaratisha asasi ya ndoa. Kwa hivyo, tumefanikisha madhumuni haya.

Madhumuni ya nne ni kuichunguza mikakati ambayo inaweza kutumiwa kuizuia asasi ya ndoa kusambaratika. Tumeona kwamba, ni muhimu kuiokoa ndoa kwani ndiyo kiini cha jamii. Tumechunguza mikakati inayotumiwa na baadhi ya wahusika katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* kuziokoa ndoa zao na kulinganisha uchunguzi wetu na ule wa wataalamu

wa masuala ya ndoa na washauri nasaha. Baadhi ya mikakati hii ni: uwazi na mawasiliano mema; kutafuta ushauri nasaha; kupata matibabu yanayofaa; kuimarisha hisia katika ndoa; kuomba na kutoa msamaha; kutilia maanani thamani ya ndoa; kuacha imani, mila na desturi zilizopitwa na wakati; uaminifu; uvumilivu; maelewano na ushirikiano. Kwa kuwa wataalamu wamependekeza mikakati hii pia, tumefaulu kufanikisha lengo hili.

## 5.2 KUHUSU NADHARIA TETE

Nadharia tete yetu ya kwanza ni kwamba, mbali na wanawake kudhulumiwa katika ndoa, wanaume pia hudhulumiwa.Tumeona waume wanawadhulumu wake zao kama vile babake Kasekesi, Agusto, Kitonga na Lusweti. Vilevile tumewaona wake wakiwadhulumu waume wao na hasa kisaikolojia. Hawa ni mke wa Mumbo kwa kumdharau, kumtusi na kumdunisha mume wake; na kuutupa mswada wake wa kitabu kwenye mvua. Mwingine ni Sasi kwa kumtusi Kaminda na kutishia kumuua. Truvessa anamdhulumu Purupesa kwa kuvichoma vitabu na mswada wake. Hii ni mifano ya dhuluma zinazotekelezwa na waume dhidi ya wake wao, na wake dhidi ya waume wao.

Nadharia tete yetu ya pili ni kuwa kila mwanandoa ana uwezo wa kuiboresha au kuisambaratisha ndoa yake. Tumeweza kuthibitisha ukweli wa nadharia tete hii katika sura ya pili ambamo tumechanganua ndoa zilizomo katika riwaya ya *Unatwa Nani?* na kutathmini mchango wa kila mwanandoa kwa kuvichunguza vitendo vyake. Tumepata kuwa wanandoa wa jinsia zote mbili wanatenda mambo chanya yanastawisha ndoa zao. Pia, wanatenda mambo hasi yanayosambaratisha ndoa zao.

Nadharia tete ya tatu ni kuwa matatizo ya ndoa hudhihirika katika matabaka yote ya kijamii. Ndoa zilizomo katika riwaya ya *Unaitwa Nani?* ni za wahusika wa matabaka mbalimbali katika jamii. Kuna wahusika wa tabaka teule kama vile, Kasina ambaye ni mfanyi biashara na mwanasiasa, babake Purupesa aliyekuwa mwanasiasa, Kassim (Wamae) ambaye ni mfanyi biashara. Wengine ni wa tabaka la kati kama vile Pasta, Kaminda, Kamene na Mumbo. Wahusika wa tabaka la chini ni kama vile wazazi wa Kamene, wazazi wa Mwanamuka, na baadhi ya wahusika wa tabaka la juu hali yao ya kiuchumi inapozorota.

Nadharia tete ya nne ni kuwa kwamba ingawa asasi ya ndoa inakumbwa na changamoto nyingi, inaweza kuokolewa isisambaratike. Tumeweza kuthibitisha ukweli wa nadharia tete hii kwa kuchunguza mikakati ambayo baadhi ya wahusika wanayoitumia kuzinusuru ndoa zao. Tumeiorodhesha mikakati hiyo katika matokeo ya madhumuni ya nne.

## 5.3 MAPENDEKEZO YA UTAFITI

Msimulizi wa riwaya ya *Unaitwa Nani?* amerejelea matini nyingine na pia dhana zinazopatikana katika matini nyingine. Pia, mwandishi hakuzingatia umbo la kimapokeo la riwaya bali ametumia mseto wa miundo ya fasihi simulizi na andishi. Tunapendekeza riwaya hii ihakikiwe kwa misingi ya mwingiliano matini. Tumepata changamoto ya kurejelea tafiti ambazo zimefanywa kutumia nadharia ya sosholojia ya fasihi kwa sababu ni watafiti wachache sana ambao wameitumia nadharia hii kuhakiki utanzu wa riwaya.

Tunapendekeza utafiti zaidi wa riwaya ufanywe kwa kutumia nadharia ya sosholojia ya fasihi.

## MAREJELEO

Albrecht, M. C. (1954) The Relationship of Literature and Society *American Journal of Sociology.*Vol. 59 No.5 Chicago: University of Chicago Press.

Amissah, A. B. (2005) "An Exploratory Study on the Self-concept and Spiritual Well-being of Commercial Sex Workers." Manila: De La Salle University. Unpublished Thesis.

Amulega, C. M. na Amulega, V. A. (2009) *Solving Problems Occuring Early in Marriage.* Nairobi: Focus Publishers.

Assembly, U. G. (1993) Declaration on the Elimination of Violence against Women. In *Proceedings of the 85$^{th}$ Plenary Meeting.* Geneva: UN

Burke, C. (2007) *Covenanted Happiness: Love and Commitment in Marriage.* Nairobi: Scepter Publishers.

Burleson, B. R. and Denten W.H. (1997) "The Relationship between Communication Skill and Marital Satisfaction: Some Moderating Effects." *Journal of Marriage and Family* Vol.59 No.4

Chalmers, F.G. (1978) "The study of Art in a cultural context": *The Journal of Aesthetics and Art criticism* Vol. 32 No. 2

Chapman, G. (2008) *Desperate Marriages. Moving toward Hope and Healing in Your Relationship*. Chicago: Northfield Publishing.

Cosbey, J. (1997) *Using Contemporary Fiction to teach family issues in Teaching Sociology* Vol. 25 No. 3 American Sociological Association.

Collins, w. na Anderson, S. (2006) *Collins English Dictionary: Complete and Unabridged.* New York: HarperCollins.

Eagleton, T. (1988) Two Approaches in the sociology of Literature: Critical Inquiry. Vol. 14 No. 3: *The Sociology of literature*. Chicago: The University of Chicago.

Encyclopaedia Britannica Online, Sv."Germaine de Stael" accessed December 03, 2011 http://www. Britannica.com/EBchecked/topic/562336/Germaine – de – stael.

Escarpit, R. (1966) *The Book Revolution.* Paris: UNESCO

__________ (1971) *Sociology of literature.* London: Frank and Cass

Gachukia, E. (1980) *The cultural conflict in East African Literature*. Tasnifu ya uzamifu Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Glicksberg, C.L. (1987) *Literature and society*: *The sociology of literature* eds. Dandson P. Cambridge: Chadwik Harley.

Goldmann, L.(1975) *Towards a Sociology of the Novel.* Cambridge: Tavistock Publications Ltd.

Greer, G.(1970) *The Female Eunuch.* Great Britain: MacGibbon & Kee Ltd.

Griswold, W. (1981) *American Character and the American Novel* An Expansion of the Reflection Theory in the Sociology of Literature. American Journal of Sociology.

Haselbarth, H. (1976) *Christian Ethics in the African Context.* Ibadan: Daystar Press.

Jadhav, A. M. (2012) The Sociology of Literature: A Study of George Orwell's *Down and Out in Paris and London. Lakavishar International E-Journal.* Vol. 1 Issue 1

Katola, E. (2006) "Udhalimu dhidi ya Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Kiswahili" Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Kiiru, M. (1978) "Aspects of the Novel in East Africa" katika Gachukia E. na Akivaga, S.K. *Teaching of African Literature in schools.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kinyua A.M. (2011) "Riwaya ya *Unaitwa nani?* Inavyoshughulikia swala la Ukombozi wa Mwanamke." Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Laurenson, D.T. na Swingewood, A.(1972) *The Sociology of Literature.* London:MacGibbon & Kee Ltd.

Longhorn (2011) *Kamusi ya Karne ya 21.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Maina, V. (2005) "Nafasi ya Mwanamke katika Tenzi mbili za Shaaban Robert: Utenzi wa Hati na Utenzi wa Adili." Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Marriage.Dictionary.Com. *Collins English Dictionary complete and Unabridged 10th edition.* Harper Collins Publishers.http://dictionaryreference.com/browse/marriage (accessed: December 12, 2011)

Mbatiah, A.M. (1999) *The Origin and Development of the Swahili Thesis Novel in Tanzania.* Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mbiti, J.S. (1991) *Introduction to African Religion.* Nairobi: East African Publishers.

Mbuthia, E.M. (2005) *A stylistic and Thematic Analysis of Kiswahili Short Stories.* Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha Nairobi.

*Merriam – Webster's Dictionary of Law*. Retrieved March 14, 2011 from Dictionary. Com website http://dictionary.reference.com/browse/marriage

Momanyi, C. (1998) "*Usawiri wa Mwanamke Mwislamu kama inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili*." Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mugambi, J. na Kirima, N. (1976) *The African Religious Heritage.* Nairobi: Oxford University Press.

Munavi, K. M. (1988) *General Psychology*. Nairobi: University of Nairobi.

Nazareth, P. (1978) *The Third World Writer: His Social Responsibility.* Nairobi. Kenya Literature Bureau.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Njue, R. M., Rombo, D. O. na Ngige L. W.(2007) *Family Strengths and Challenges in Kenya*. New York:The Harworth Press.

Ntarangwi M. (2004) *Uhakiki wa kazi ya Fasihi.* Rock Island: Augustana College

Nyaosi, K.N. (2008) "Taswira ya Asasi ya Ndoa katika Riwaya mbili za Kiswahili *Kiu* na *Msimu wa Vipepeo*." Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Orina, B.M. (2000) "Utetezi wa Maadili katika Fasihi – Nadhari ya Shaaban Robert." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa

Osoro, G.M. (2003) "Uhakiki wa Riwaya za Said Ahmed Mohamed kwa Misingi ya Kifeministi." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa

Republic of Kenya (1962) *The Matrimonial Causes Ordinance ( Chapter 152)*. Nairobi: The Government Printer.

________________(2010) *The Constitution of Kenya, 2010* Kenya Gazette Supplement. Nairobi: The Government Printer.

Rogers, M.F. (1991) *Novels, Novelists and Readers. Towards a Phenomenological Sociology of Literature.* New York: State University of New York.

Stael, M. de (1803) *A Treatise on Ancient and Modern Literature*. London: G. Cawthorn

__________(1835) *The Influence of Literature upon Society*. New York: W. Pearson & co.

Sullivan, T. A. (1982) *Introductory Sociology Through Literature*. Teaching Sociology. American Sociological Association 10(1)

Swingewood, A. (1975) *The Novel and Revolution.* London: The Macmillan Press Ltd.

Thiong'o N. (1978) "Literature in Society" in Gachukia E. na Akivaga, S.K. (ed) *Teaching of African Literature in Schools*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi. Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

____________ (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Books.

____________ (2005) "Mahojiano Mafupi na Lutz Diegner juu ya Riwaya ya *Bina—Adamu!*" (2002) *Swahili Forum* 12 Uk. 95 – 97.

____________ (2007) *Dharau ya Ini.* Nairobi: Vide – Muwa Publishers.

____________ (2008) *Unaitwa Nani?* Nairobi: Vide – Muwa Publishers.

Weitzer, R. (2000) "Why We Need More Research on Sex Work" in R. Weitzer(ed) *Sex for Sale: Prostitution, Pornography And the Sex Industry*. New York: Routledge.

Wellek, R. na Warren, A. (1978) *Theory of Literature.* London: Penguin Books.